
UKURASA 20



## Sikia mpya ya Gigy Money

## RC: Tekelezeni miradi yenye tija



UKURASA 4

## MAISHA

Machi 7, 2021 Nipashe — Baba, Mama na Mwana — Jumapili



HARUSI

Ukurasa 12



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**

PAZIA kupendezesha nyumba

**Mkate wa mayai**

Ukurasa 14






# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Machi 7, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

www.ippmedia.com

ISSN 0856 • No. 0580512


# Mgodi mkubwa wa dhahabu kufungwa

UKURASA 3



Wanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Bugosi, Kata ya Nyamisangura, wilayani Tarime, mkoani Mara, wakiwa darasani huku baadhi yao wakiwa wameketi chini hivi karibuni, kutokana na upungufu wa madawati. Picha ndogo: Baadhi ya walimu wa shule hiyo, wakisahihisha madaftari nje kwenye varanda kutokana na kutokuwapo kwa ofisi ya walimu. **PICHA: DINNA MANINGO**

UKURASA WA 3

## MABORESHO BANDARI YALETA NEEMA

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA), Deusidedit Kakoko, amesema maboresho makubwa...

## Maajabu ya tango kudhibiti magonjwa

UKURASA 7

# Mume, mke walivyopoteza maisha gari likizama mtoni

UKURASA 2

**MICHEZO** **MGOSI AIPONDA YANGA PRINCESS, AONGOZA LIGI** UK. 23

MAONI, KATUNI UK.6

# Mume, mke wafariki dunia gari likisombwa na maji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KAIMU Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Kanda ya Kati, Dk. Aluna Chawala, na mkewe Neema Mwasanganga,wamefariki dunia kwa kusombwa na maji katika Daraja la Shaaban Robert wilayani Mpwapwa mkoani Dodoma wakati wakijaribu kujiokoa baada ya gari lao kuzima katikati ya maji.

Akizungumza na Nipashe jana kuhusu tukio hilo, Mkuu wa Wilaya ya Kongwa ambaye ni Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Dk. Suleiman Serera, alisema ajali hiyo ilitokea juzi majira ya saa moja usiku katika daraja hilo.

Dk. Serera alisema inadaiwa Dk. Chawala alikuwa akimpeleka mkewe kazini katika Hospitali ya Wilaya ya Mpwapwa ambako alikuwa na zamu ya usiku.

Alisema wawili hao walikuwa wakitumia gari aina ya Nissan Xtrail lenye namba za usajili T 483 BRR ambalo lilizimika katika eneo hilo la daraja kutokana na kuzidiwa na maji.

Alifafanua kuwa kwa mujibu wa mashuhuda, Dk. Chawala baada ya kuona hali hiyo, alishuka na kuanza kutembea huku akimwambia mkewe ashuke ili wavuke, lakini mkewe alishindwa kutokana na maji kuongezeka katika eneo hilo.

Dk. Serera alisema kuwa baada ya kuona hali hiyo, Dk. Chawala alirudi ili kumwokoa mkewe ndipo maji yakawazidi nguvu na kuwasomba kuwadondoshea ndani ya daraja hilo pamoja na gari lao.

“Chini ya daraja kuna mawe, hivyo miili ya marehemu imepatikana ikiwa na michubuko kutokana na kujigonga.

“Uokoaji umefanywa na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na vikosi vingine kwa kushirikiana na wananchi na tumefanikiwa kutoa maiti na gari,” alisema.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania, Dk.Jonas Kizima, alisema tukio hilo limewasikitisha kutokana na kupoteza nguvu kazi ya taasisi hiyo.

Alisema miili ya wanandoa hao imehifadhiwa katika Hospitali ya Mpwapwa ikisubiri taratibu za mazishi zinazofanywa na ndugu kwa kushirikiana na serikali.

Alisema miili hii inatarajiwa kusafirishwa leo kwenda Kilolo mkoani Iringa kwa ajili ya maziko.

Kamanda wa Polisi mkoani Dodoma, Girres Muroto, pia alithibitisha kutokea kwa vifo hivyo, akiwataka wananchi kuchukua tahadhari dhidi ya maji.

Kamanda Muroto alibainisha kutokea tukio lingine Kibaigwa wilayani Kongwa na kusababisha kifo cha Stella Christopha (42), fundi cherehani na mtoto mdogo aliyekuwa amembeba mgongoni, Elia Justine.

Vifo hivyo vimetokea baada mama huyo kusombwa na maji yaliyokuwa yanatiririka katika mto ambao walikuwa wakivuka.



Mabaki ya gari aina ya Nissan Xtrail, lenye namba za usajili T483 BRR, lililozimika katika eneo hilo la daraja na kuzidiwa na maji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Marehemu Dk. Aluna Chawala



Marehemu Neema Mwasanganga

# Mgodi mkubwa wa dhahabu kufungwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MGODI wa Buzwagi ulioko Kahama mkoani Shinyanga, unatarajia kufunga shughuli za uzalishaji wa madini Juni, mwaka huu.

Meneja wa Ufungaji wa Mgodi na Mazingira wa mgodi huo, Rebecca Stephen, alibainisha hayo jana alipotoa taarifa ya ufungaji wa mgodi huo kwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana na Ajira), Patrobas Katambi, aliyezuru mgodini huko.

Rebecca alisema ifikapo June mwaka huu, mgodi utafunga uzalishaji wake na kuanza hatua ya kurudisha mazingira yalivyokuwa awali.

Alisema kuwa hivi karibuni watawasilisha mpango mpya wa kufunga mgodi katika Tume ya Madini. Hata hivyo, yapo masharti ya kisheria yanayoweka udhibiti katika ufungaji wa mgodi.

Rebecca alisema mgodi umekuwa ukiendelea kutoa elimu ya ujasiriamali, utunzaji wa fedha kwa wafanyakazi wa mgodi ili kuwa na matumizi sahihi ya fedha na kujikita katika biashara baada ya mgodi kufunga shughuli zake.

Alisema wanafundisha namna ya kuhuhisha wasifu wa kitaaluma (CV) na kuwasaidia wafanyakazi wao kupata ajira sehemu nyingine na kwamba ikitokea kazi katika Mgodi wa Bulyanhulu, wanawapatia kipaumbele wafanyakazi waliokuwa Buzwagi kwanza.

Meneja huyo alisema utaratibu huo umesaidia kupunguza makali ya kukosa ajira kwa waliokuwa wafanyakazi katika Mgodi wa Buzwagi.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana na Ajira), Katambi, baada ya kupewa taarifa hiyo, aliutaka uongozi wa mgodi huo, kusimamia vyema sheria za kazi na kuhakikisha unawalipa stahiki wafanyakazi wake, ili kuondoa migogoro iliyoanza kujitokeza.

“Kuandaa malipo ya wafanyakazi hawa mapema kutasaidia kuzibana kampuni zilizopo ndani kulipa stahiki za wafanyazi wao.

“Msipofanya hivyo, watatokomea kusikojulikana na maslahi yao yatapotea kwa kuwa hakuna mhusika kwa wakati huo,” Katambi alitahadharisha.

Alibainisha kuwa wafanyakazi 253 kukosa ajira si jambo jema, hivyo akavitaka vyama vya wafanyakazi vianze kushughulikia malipo yao mapema.

Katambi alisema wahusika wanapaswa kulipa fedha za michango ya wafanyakazi kwenye Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF) na kodi za serikali.

Naibu waziri huyo pia aliagiza kuwa wakati wa kufunga mgodi unapaswa kwenda sambamba na kukusanya mali na kulipa madeni.

Akiwa kwenye Mgodini wa Bulyanhulu, Katambi aliwataka viongozi kuhakikisha matangazo yote ya ajira yanayohusu mgodi huo, kuwekwa kwenye mbao za matangazo ambazo zipo katika maeneo yanayozunguka mgodi, ili wananchi wenye ujuzi waombe ajira hizo.

Katambi alisema viongozi wa mgodi huo wanao wajibu wa kutoa matangazo ya ajira kwa wananchi wanaozunguka mgodi, ili wananchi waombe kazi na kuondoa malalamiko ya migodi kuajiri watu kutoka nje ya nchi na mikoa jirani.

“Tuna vijana wengi mitaani wanaozunguka migodi hii hawana ajira na wana ujuzi mbalimbali. Wanashindwa kuomba ajira kutokana na kutoona matangazo ya ajira.

“Kwa kutambua hilo, ninaagiza matangazo yote ya ajira yabandikwe kwenye mbao za mtangazo vijijini na ofisa za watendaji wa kata,” aliagiza.

Mbunge wa Msalala, Idd Kassimu, alidai kuna ukiritimba mkubwa katika ajira zinazotolewa na mgodi kwenda kwa wananchi wanaozunguka maeneo hayo.

Alisema hicho ndicho kiini cha uhusiano mbaya baina ya mgodi na wananchi wanaozunguka.

Kaimu Meneja Mkuu wa Mgodi wa Bulyanhulu, Zumbi Musiba, alisema wamepokea maelekezo hayo ya serikali na watayafanyia kazi kwa haraka, ili kuondoa malalamiko.

Aliwataka wananchi kutokuwa na wasiwasi kuhusu suala hilo kwa kuwa wao ndiyo majirani zao na lazima wawe karibu nao.

Januari 18, 2017, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ilizuru katika Mgodi wa Buzwagi na kubaini kuwa mwaka 2012, mgodi huo ulikuwa na wafanyakazi 1,084, lakini mwaka 2016 walipunguzwa 362, hivyo kubaki na waajiriwa rasmi 722.

Kati ya waajiriwa hao 722, waajiriwa 715 walikuwa wazawa wakati wafanyakazi wa kigeni walikuwa saba na kwamba sababu ya punguzo hilo ni kushuka kwa uzalishaji.

Mgodi wa Buzwagi ni miongoni mwa migodi mitatu ya dhahabu Kanda ya Ziwa inayomilikiwa na Kampuni ya Barrick. Mingine ni Bulyanhulu uliopo Kahama pamoja na North Mara uliopo Nyamongo mkoani Mara.

Mgodi wa Buzwagi uligunduliwa mwaka 1950 lakini uchimbaji na upatikanaji wa dhahabu ulianza mwaka 2009 na ulitarajiwa kufungwa mwaka 2019.

Mwaka 2009 wakati mgodi huo unafunguliwa kwa uwekezaji wa Dola za Marekani milioni 400 (sawa na Sh. bilioni 888), ulitarajiwa kuajiri wafanyakazi zaidi ya 3,000.

## HABARI KITAIFA

# Silinde abaini tatizo kwa wahandisi

**Na Thobias Mwanakatwe**

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, amesema wahandisi wa halmashauri nchini wanaongoza kwa kuikosea serikali kutokana na kushauri vibaya kitaalamu katika miradi ya ujenzi na kuweka gharama za juu.

Alisema hayo jana baada ya kutembelea miradi ya ujenzi wa mabweni katika Halmashauri za Bariadi na Itilima mkoani Simiyu.

Silinde alisema kutokana na ushauri mbaya unaotolewa na wahandisi hao, miradi mingi haikamiliki kutokana na kutozingatia bajeti inayopangwa na serikali kuu. Katika miradi ya ujenzi wa mabweni inayojengwa katika halmashauri hizo, Silinde alikuta haijakamilika huku wahandisi wakilalamikiwa kwa kutoa makisio ya bei za juu za ujenzi kuliko hali halisi ya ujenzi.

"Nimepita katika halmashauri zingine gharama ile tuliyotoa ya Sh. milioni 80 imemaliza ujenzi kwa kuwa baadhi ya wakuu wa shule walibana matumizi na kusimamia vizuri fedha walizopewa," alisema.

Silinde alisema kuwa katika maeneo mengine, wengi walioshindwa kumaliza, walifuata ushauri wa wahandisi wasio wazalendo kwa serikali yao, ambao walipotosha na kuweka gharama kubwa zaidi na kufanya walimu kuingia matatizoni kwa matumizi mabaya ya fedha.

Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, Festo Kiswaga, amemwahidi Silinde kuwa mpaka ifikapo Mei, mwaka huu, majengo yote ya mabweni yatakuwa yamekamilika kwa fedha za ndani baada ya fedha walizoletewa na serikali katika shule mbili wilayani kwake kwa ajili ya ujenzi wa mabweni Sh. milioni 160 kushindwa kumaliza mradi huo.

Katika hatua nyingine, Silinde aliwaagiza wakuu wa shule za sekondari za Itilima, Bariadi na Nyasosi na maofisa elimu sekondari wilaya za Bariadi na Itilima kuandika barua kujieleza kwanini wasichukuliwe hatua kwa kuchelewa kumaliza ujenzi wa mabweni katika shule hizo.

Silinde alisema endapo watashindwa kukamilisha majengo hayo kwa muda walioomba kuongezewa, basi atawavua nyadhifa zao.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi akimsikiliza Mkurugenzi Mkuu wa Kiwanda cha sukari Mahonda Zanzibar, Rahim Bhaloo, alipofanya ziara yake kuangalia uzalishaji wa sukari, jana. **PICHA: IKULU**

# Walengwa TASAF watoka kwenye umaskini

**Na Marco Maduhu**, BUSEGA

WALENGWA wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) wilayani Busega mkoani Simiyu, wameondokana na umaskini kupitia fedha za Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini.

Mmoja wa walengwa hao, Kulwa Pigahapa kutoka Kijiji cha Chamugasa, alisema juzi kuwa fedha za mpango huo zimemtoa kwenye umaskini.

Alisema kupitia uwekezaji alioufanya kwa kutumia fedha za mpango huo, sasa nyumba za bati, ng'ombe wanne, kondoo 10 na anamiliki shamba la miwa ekari moja na nusu.

"Awali, maisha yangu yalikuwa magumu sana. Nilikuwa ninaishi kwa vibarua, kula kwa shida na kukodi mashamba, lakini sasa maisha yangu yamebadilika, siyo maskini tena," alisema Pigahapa.

Rahel Nicolaus, mlengwa mwingine wa TASAF kutoka Kijiji cha Kabita, alisema alikuwa anaishi kwa majirani baada ya nyumba yake ya tope kuanguka kutokana na mvua, lakini sasa amejenga nyumba imara kupitia fedha za TASAF na anamiliki mbuzi watano.

Ofisa Ufuatiliaji wa TASAF wilayani Busega, Gibanga Makoba, alisema asilimia 85 ya walengwa wilayani humo maisha yao ni mazuri.

Alisema walengwa hao sasa wamejenga nyumba imara, wana mashamba na mifugo.

Ofisa huyo alibainisha kuwa wilayani humo kuna walengwa 3,300 wa mfuko huo na kwamba tangu kuanza kwa mpango huo mwaka 2015, wameshatoa Sh. bilioni 4.9 kwa ajili ya kuzinusuru kaya maskini.

# Maboresho bandari ya Kigoma yaleta neema

**Na Mwandishi Wetu,** KIGOMA

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA), Deusidedit Kakoko, amesema maboresho makubwa yaliyofanywa katika Bandari ya Kigoma, yameanza kuleta matokeo chanya ikiwamo kuongeza shehena ya mizigo na mapato. Akizungumza na waandishi wa habari jana katika bandari hiyo, Kakoko alisema shehena na mapato yake sasa yameizidi Bandari ya Mwanza ambayo awali ndiyo iliyokuwa ikiongoza kabla ya maboresho hayo.

Alisema Bandari ya Kigoma ambayo inahusisha bandari zote zilizoko katika Ziwa Tanganyika, imeanza kufanyiwa maboresho kuanzia mwaka 2016/17 ikihusisha ujenzi wa magati, ununuzi wa mitambo, ujenzi wa maghala na majengo ya abiria pamoja na ujenzi wa ofisi za kisasa za makao makuu ya bandari hiyo ambazo ziko katika hatua za mwisho kukamilika.

Aliongeza kuwa maboresho hayo yanafanyika kutokana na kasi kubwa ya ongezeko la mahitaji ambayo hayakuendana na miundombinu iliyokuwapo awali.

Alisema bandari za Ziwa Tanganyika zimekuwa kiungo kikubwa cha biashara kati ya Tanzania na nchi jirani za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Burundi na Zambia, huku biashara kubwa ikiwa ni mazao yanayozalishwa Tanzania.

Kakoko alisema bandari hizo zimekuwa kichocheo kikubwa cha kukuza uchumi wa wananchi wa mikoa inayozunguka Ziwa Tanganyika kutokana mazao yao kupata idadi kubwa ya wanunuzi wanaotokana na matumizi ya bandari hiyo.

Pia, alisema matumizi ya bandari hiyo yamesaidia kupunguza bei za bidhaa ambazo gharama zake zimekuwa zikipanda kutokana na gharama kubwa za usafirishaji.

Kakoko alisema bado kuna maboresho zaidi yanaendelea katika Bandari ya Kigoma yanayohusisha ujenzi wa gati ya boti ya Kibirizi, gati ya abiria na makasha pamoja na ujenzi wa bandari kavu ya Katosho.

"Tumekusudia kuifanya Bandari ya Kibirizi na Kigoma kuwa ya mizigo ya nje na ile ya Katosho itakuwa ya ndani, " alisema Kakoko.

Alisema matarajio ya kuongezeka zaidi kwa shehena na abiria ni makubwa kutokana na maboresho ya meli yanayotarajiwa kufanywa na Kampuni ya Huduma za Meli zikiwamo MV Mwongozo, MV Liemba na MV Sangara.

# COSTECH: Elimu itatue matatizo katika jamii

**Na Christina Mwakangale**

MKURUGENZI Mkuu wa Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), amewataka wadau wa elimu na jamii kuwaandaa vijana ili kuitumia elimu wanayoipata shuleni hususan somo la sayansi, kutatua matatizo kwenye jamii.

Dk. Amos Nungu alitoa rai hiyo Dar es Salaam jana alipozindua mradi wa Future STEM Business Leaders (FSBL) kupitia Atamizi ya Teknohama ya Dar es Salaam (DTBi).

Alisema mradi huo ambao ulianza mwaka 2017 kupitia DTBI, ambayo ina uzoefu wa kuwajengea uwezo vijana kubuni na kukua kibiashara, ukifanyika kwenye shule 13 zikiwamo nane za Dar es Salaam na tano Arusha.

Dk. Nungu alisema mradi huo utawajengea uwezo wanafunzi hao kupitia masomo ya sayansi, kubaini fursa kujiajiri na kuajiri.

Alisema kutokana na dunia kukua kidigitali, ipo haja wanafunzi kuandaliwa tangu sekondari badala ya kusubiri wafike chuo kikuu.

"Mradi unasimamiwa na COSTECH kupitia DTBi, umefadhiliwa na Idara ya Fizikia ya Uingereza. Unatekelezwa pia tukishirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Idara ya Fizikia na Arusha Tech," alisema.

Dk. Nungu alitoa wito kwa vijana kuwa sehemu ya utatuzi wa matatizo yaliyopo kwenye jamii kwa kutumia teknolojia.

"Msiikimbie sayansi, vijana wengi wanakuja na mawazo yenye ubunifu lakini hayafanyiwi kazi. Kupitia mradi huu, wataibuliwa wenye wazo zuri ambalo ni la kibiashara na kusaidia jamii," alisema Dk. Nungu.

Meneja Mradi wa FSBL-DTBi, Josephine Sepeku, alisema unahusisha wanafunzi na walimu wa sayansi kubuni wazo ambalo litaboreshwa na kuwa bidhaa.

"Tuna shule nane za Dar es Salaam kwenye mradi pia tano kutoka Arusha. Tunawapa elimu ya ziada kufanya sayansi wanayoisoma kuwa biashara kupitia ubunifu wao," alisema Josephine.

Ofisa Utafiti Mwandamizi kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Rodgers Msuya, alisema wizara inatambua mchango wa mradi huo katika kukuza sayansi na vipaji.

"Tutashirikiana kwa namna yoyote tutakapohitajika, ili kuhakikisha sayansi inakuwa biashara miongoni mwao vijana," alisema Dk. Msuya.



Waziri wa TAMISEMI, Selemani Jafo (kushoto), akipata maelezo kwa Mhifadhi Mazingira kutoka Mfuko wa Wanyamapori Duniani (WWF), Dk. Severin Kalonga, alipotembelea banda la Vodacom na WWF, katika maonyesho ya Tamasha la Kisarawe Ushoroba, linalotangaza vivutio vya utalii kwenye hifadhi ya msitu wa mazingira asilia wa Kazimzumbwi, tamaduni za Wazaramo na hifadhi mpya ya Taifa ya Mwalimu Nyerere, wilayani Kisarawe, mkoani Pwani jana. Kulia ni Meneja wa Vodacom Tanzania Foundation, Sandra Oswald. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# RC: Tekelezeni miradi yenye tija

**Na Maulid Mmbaga**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abubakar Kunenge, amewataka viongozi ndani ya mkoa huo kutekekeza miradi yenye tija na uhitaji wa haraka kwa wananchi.

Alitoa agizo hilo juzi katika kikao na Bodi ya Barabara uliowajumuisha Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) pamoja na wakuu wa wilaya, wakurugenzi, madiwani na wabunge wa majimbo yaliyopo ndani ya mkoa huo.

Kunenge alisema kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi kuwa kuna maeneo yanahitaji utekelezaji wa haraka wa miradi kwa kuwa shughuli za kimaendeleo zinakwama.

Alisema serikali imejipanga na imedhamiria kuboresha miundombinu ya mkoa huo, lakini kuna baadhi ya sehemu kumetekelezwa miradi isiyo na tija kwa wakati uliopo.

"Tunapotaka kutekeleza miradi hasa inayohusu barabara. Tuangalie vipaumbele muhimu vinavyozingatia mahitaji ya wananchi, kwani kuna sehemu kuna changamoto lakini hazijatatuliwa na pesa zimepelekwa mahali ambapo hapana tija," alisema.

Kunenge alisema kuna baadhi ya viongozi wamekuwa wabinafsi, jambo lililosababisha wapate shida katika kutatua baadhi ya matatizo kwa kuwa fedha zilipelekwa katika sehemu zisizokuwa na ulazima kwa wakati uliopo.

Mratibu wa TARURA Mkoa wa Dar es Salaam, Geofrey Mkinga, alisema wako kwenye utekelezaji wa Mradi wa Uendelezaji Jiji la Dar es Salaam (DMDP) unaojumuisha ujenzi wa jumla ya Km 64.74 za barabara za lami, soko moja na vituo vya kukusanywa taka ngumu vitatu.

Mingine ni ujenzi wa kingo za Mto Chang'ombe na Kiboko Km 11.2 ili kuzuia mafuriko ya mara kwa mara, maeneo ya kupumzika na vyoo vya umma pamoja na ujenzi wa jengo la ghorofa moja, vyote vikigharimu Sh. bilion 205.777.

Alisema mafanikio ya mradi huo ni ongezeko la ajira kwa wananchi hasa kwenye maeneo mradi unapotekelezwa sambamba na kuchochea biashara kufanyika.

"Mradi haukuhusisha halmashauri za Ubungo na Kigamboni kwa kuwa hazikuwa zimeundwa. Kwa ujumla, utekelezaji wa mradi wa DMDP katika awamu ya kwanza umefikia kiwango cha asilimia 88 na unatarajiwa kukamilika Juni 2022," alisema.

Meneja wa TANROADS Mkoa wa Dar es Salaam, Tenga Eliamin, alisema kuwa mwaka huu wa fedha, wakala huo umepanga kutumia Sh. bilion 48 na kati yake, Sh. bilioni 26.8 zinatumika katika matengenezo ya barabara.

"TANROADS pia inasimamia ujenzi wa barabara katika jiji hili ili kupunguza foleni ikiwa ni pamoja na upanuzi wa Barabara ya Morogoro Km 32 sambamba na barabara ya mwendokasi na ujenzi wa madaraja katika makutano," alisema.

# TBS yaita wafanyabiashara usajili majengo

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Viwango (TBS) limewataka wafanyabiashara kujitokeza kusajili bidhaa na majengo ya vyakula na vipodozi, ili kuwawezesha kufanya shughuli zao kwa kukidhi matakwa ya sheria za nchi na kulinda afya za walaji.

Wito huo ulitolewa na Ofisa Uhusiano wa Shirika hilo, Neema Mtemvu, kwenye maonyesho ya wafanyabiashara wanawake Tanzania yaliyofanyika Mlimani City, Dar es Salaam jana.Maonyesho hayo yalianza Machi 4 mwaka huu, TBS ikishiriki na kutoa elimu kuhusu masuala mbalimbali ya viwango kwa wananchi, wajasiriamali, wafanyabiashara na wadau mbalimbali waliofika kutembelea maonyesho hayo.

Alisema msisitizo wao ni kuwataka wafanyabiashara kusajili bidhaa na majengo ya vyakula na vipodozi kwa mujibu wa sheria, ambayo imetokana na mabadiliko ya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2019.

Sheria hiyo ilirudisha majukumu ya usimamizi wa usalama na ubora wa vyakula na vipodozi kwa TBS kutoka kwa iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA).

Alisema kwa msingi huo, usajili wa bidhaa, majengo ya vyakula na vipodozi ni matakwa ya kisheria ili kuwawezesha kufanya biashara zao kwa urahisi.

Ofisa huyo alisema usajili wa majengo ya biashara unawapa wafanyabiashara uhakika wa kutunza bidhaa na wanasajili jengo kulingana na bidhaa zinazoenda kuhifadhiwa humo.

Katika usajili wa bidhaa, Mtemvu alisema eneo linalohusika ni bidhaa za chakula na vipodozi.

Alisema usajili wa vipodozi unalenga kuhakikisha vipodozi vilivyopigwa marufuku kwenye soko la Tanzania, haviingizwi nchini kutokana na kuwa na viambata sumu.

Katika hatua nyingine, Mtemvu alitoa wito kwa wajasiriamali kujitokeza kuthibitisha ubora wa bidhaa zao TBS bila malipo kwa kuwa gharama hizo zinalipwa na serikali.

Kwa mujibu wa Mtemvu, wanachotakiwa kuwa nacho, ni barua ya utambulisho kutoka Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) na baada ya hapo wakifika TBS mchakato unaanza mara moja.

MAKALA MAALUM

# TARURA inavyozisuka barabara za Ruvuma

**Bebi Kapenya na Thereza Chimagu,**
SONGEA

UNAPOTAJA uzalishaji wa nafaka Tanzania, bila shaka ni vigumu kutotaja Ruvuma. Mkoa huo unaosifika kwa uzalishaji mkubwa wa mahindi.Wakati Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) unaendelea kutekeleza majukumu yake ya kufanya matengenezo na maboresho ya miundombinu ya barabara, madaraja na vivuko katika mikoa mbalimbali nchini, Mkoa wa Ruvuma haujaachwa nyuma katika hilo.

TARURA wanaendelea na majukumu hayo kwa lengo la kuifanya miundombinu hiyo kuwa katika hali nzuri kwa kipindi chote cha mwaka kwa lengo la kuwezesha wananchi kusafiri na kusafirisha bidhaa na mazao yao kwa haraka na kwa gharama nafuu. Katika Mkoa wa Ruvuma ambao makala hii inauangazia, TARURA imekuwa ikihakikisha miundombinu ya barabara hasa mashambani inapitika ili kurahisisha usafirishaji wa mazao ya wakulima yanafika sokoni haraka kwa lengo la kuinua uchumi wa wananchi.

Akizungumza katika mahojiano maalum, Mratibu wa TARURA Mkoa wa Ruvuma, Edward Lemelo, anabainisha kuwa tangu TARURA ianzishwe, katika Mkoa wa Ruvuma kwa asilimia 30 mtandao wa barabara una hali nzuri kwa maana zinazopitika mwaka mzima.“Tumefanya matengenezo mengi kwa maana ya matengenezo ya kawaida (Routine Maintenance) zaidi ya Km 1291.7, matengenezo ya sehemu korofi (Spot Improvement) sehemu zilizokuwa zinasumbua wananchi zaidi ya Km 540, tumefanya matengenezo ya muda maalum yaani matengenezo makubwa (Periodic Maintenance) zaidi ya Km 665 pamoja na kujenga madaraja madogo na makalavati 633 katika barabara mbalimbali za TARURA kwenye mkoa wetu,” anasema.

Lemelo anasema TARURA Mkoa wa Ruvuma imetekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, wakala umejenga daraja kubwa la Fundimbanga lenye urefu wa mita 45 kwa Sh. bilioni 1.5 na sasa wananchi wa eneo hilo wanapita bila shida tofauti na awali. “Ukitoka kwenye barabara kubwa kuna kijiji kinaitwa Tabora mpaka kufika kijiji cha Fundimbanga, wananchi walikuwa hawawezi kutoka kwenye vijiji hivyo kufika mjini hasa kipindi cha masika, lakini tumewezesha wananchi kufikia barabara kubwa kwa kutumia daraja hilo ili waweze kusafirisha mazao yao kwa urahisi,” anasema.



Mwonekano wa Barabara ya Tunduru-Seed Farm yenye urefu wa Km 1.25 iliyojengwa na TARURA katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma.

Kwa mujibu wa Mratibu huyo, Halmashauri ya Wilaya ya Madaba ambayo ni mpya, haikuwa na barabara lami lakini sasa wamejenga barabara ya Madaba-LITA Km moja kwa kiwango cha lami na kuweka taa za barabarani.

Pia kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara, wamejenga Barabara ya Kona Bar-NMB-Makalavati Juu kwa kiwango cha lami yenye urefu wa mita 750 na wanaendelea na ujenzi wa barabara ya Wino-Ifinga-Luhuji kwa kiwango cha changarawe Km 15.

Kwa Halmashauri ya Wilaya ya Songea, utekelezaji wa miradi mbalimbali umefanyika ikiwamo ujenzi wa barabara ya Peramiho-Lundusi Km 6.43 na Peramiho-Morogoro Km 7.34, zote kwa kiwango cha lami na barabara hizo zimesaidia wananchi kutoka katika vijiji vya Morogoro na Peramiho kuifikia Hospitali ya Peramiho kwa urahisi zaidi.

Anasema kwa sasa wako katika maandalizi ya ujenzi wa Daraja la Mto Muhukulu mradi ambao bado upo katika hatua ya usanifu na ujenzi unatarajia kuanza hivi karibuni.



Mwonekano wa Barabara ya Peramiho-Morogoro-Nakahuga yenye urefu wa Km 7.34 iliyojengwa na TARURA katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma.

Katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea, wamejenga barabara kwa kiwango cha lami Km 12.3 na kuweka taa za barabarani kwa kutumia Mradi wa Uimarishaji Halmashauri za Miji (ULGSP).

Mratibu huyo pia anasema kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara, wamejenga barabara ya lami (Tunduru Seedfarm) Km 0.75, barabara ya Pachanne-Mjimwema kwa kiwango cha lami nyepesi Km 0.4 na barabara ya Seedfarm kwa kiwango cha Changarawe Km tatu na pia wanaendelea kujenga Km moja za lami kila mwaka ili kuuboresha mji huo.

Lemelo anasema kuwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, wamejenga barabara ya Mbinga-Litoho kwa kiwango cha Lami Km 25 ambayo hapo awali ilikuwa na hali mbaya kwa kuwa wananchi walikuwa wanatembea wiki nzima kusafirisha mazao yao.

“Kuna sehemu inaitwa Litoho ambapo ni mpakani mwa Nyasa na Mbinga, kule kuna wananchi wengi ambao ni wakulima wa mazao ya kahawa na ndizi walikuwa wanatumia wiki moja kuleta mazao yao mjini, lakini baada ya kuweka lami kwa sasa wanatumia dakika 30 tu kufika mjini na kuuza mazao yao kwa urahisi.

“Kwa hiyo, ujenzi wa barabara hii umesaidia sana wakulima kusafirisha mazao yao kwa urahisi na kwa gharama nafuu,” anasema mratibu huyo.

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa, TARURA imejenga daraja kubwa la Tingi-Lulimbo-Mtuha na kufungua barabara Km 15 katika barabara ya Tingi-Lulimbo-Mtuha ambayo imesaidia wananchi kuvuka kutoka Nyasa kwenda Wilaya ya Mbinga kwa kutumia njia fupi na kusafirisha mazao yao kwa haraka kupeleka sokoni.

Vilevile, wamejenga barabara ya Tumbi-Mango-Kindili kwa kutumia zege (concrete strips) Km 15 sehemu ambayo ilikuwa korofi lakini baada ya ujenzi wa barabara hiyo, imewasaidia wananchi kuzifikia huduma za afya kwa urahisi.

TARURA katika Halmashauri ya Mji wa Mbinga imefanya matengenezo ya barabara ya Lipembe yenye urefu wa Km 32.61 kwa kiwango cha changarawe na barabara ya Mpepai-Kihungu Km 16.50 na Pachasita-Tulila Km 10.66 kwa kiwango cha lami.

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, wakala huo umeboresha barabara iitwayo Libango-Kiburungutu-Mtumbatimaji kwa kiwango cha changarawe Km 10 barabara ambayo inatoka katika Kijiji cha Libango kwenda mjini.

Mkazi wa Kijiji cha Fundimbanga Wilaya ya Tunduru, Alto Luambano, anaipongeza TARURA kwa kutengeneza daraja kubwa la Fundimbanga lenye urefu wa mita 45 ambalo limesaidia kusafirisha mazao na hivyo kufika sokoni kwa urahisi.

“Kabla ya ujenzi wa daraja hili, wananchi wa vijiji vya Tabora na Fundimbanga tulipata shida katika kusafirisha mazao yetu, lakini TARURA wametuondolea hilo tatizo kwa kututengenezea daraja,” anasifu Luambano.

Jeremiah Makelele, mkulima wa maharage Kata ya Wino, Halmashauri ya Madaba, anasema katika kata yao wanalima maharage, mahindi, ndizi, mpunga, tangawizi na uvunaji wa mazao ya misitu.

Anasema eneo hilo pia lina shughuli za kijamii kama vile shule na vituo vya afya, hivyo mahitaji ya miundombinu bora na ya uhakika ni muhimu sana na anaipongeza TARURA kwa kuanza ujenzi wa barabara ya Wino-Ifinga-Luhuji yenye urefu wa Km 15 kwa kiwango cha changarawe ambayo itawasaidia kusafirisha mazao yao kwa urahisi.

Happy Sawali, mkazi wa Peramiho Wilaya ya Songea, anaipongeza serikali kupitia TARURA kwa kutengeneza ya barabara ya Peramiho-Lundusi Km 6.43 na Peramiho-Morogoro Km 7.34, zote kwa kiwango cha lami kwa kuwa zimerahisisha usafiri na kusaidia wananchi kutoka katika vijiji vya Morogoro na Peramiho kufikia Hospitali ya Peramiho kwa urahisi.

Mkoa wa Ruvuma una mtandao wa barabara wenye jumla ya Km 7,143.7 ambao unahudumiwa na TARURA na kati ya hizo, Km 82.2 ni barabara za lami ambazo ni asilimia 1.2 ya mtandao mzima, Km 937 ni barabara za changarawe ambazo ni asilimia 11.7 ya mtandao mzima na Km 6,124.5 ni barabara za udongo ambazo ni asilimia 87.1 ya mtandao mzima.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Upimaji afya upewe msisitizo kuokoa maisha ya Watanzania

**MATATIZO** ya afya yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku huku baadhi ya ripoti zinazotolewa na wataalamu wa afya zikiwa zinatisha au kukatisha tamaa.

Miongoni mwa maradhi ambayo yamekuwa yakiongezeka kwa kasi na hata kusababisha baadhi ya watu kupoteza maisha ni yale yasiyo ya kuambukiza kama vile saratani, shinikizo la damu, kisukari na uzito uliozidi kiwango.

Kutokana na hali hiyo watalaamu wa afya pamoja na viongozi katika maadhimisho ya magonjwa mbalimbali, wamekuwa wakihimiza watu kupima afya zao ili kutambua hali zao na hatimaye kuchukua hatua.

Pamoja na msisitizo huo, watu wengi bado wamekuwa na mwamko mdogo katika kuitikia wito huo na hatimaye kujikita wakipatwa na matatizo ya kiafya na hata kupotesha maisha. Mara nyingine, wamekuwa wakienda kupata huduma za afya wakiwa katika hali mbaya au hatua za mwisho huku maradhi hayo yakiwa yameshambulia sehemu kubwa za miili yao.

Hivi karibuni, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) ilitangaza watu kujitokeza kwa wingi kupima afya bure viwanja vya Zakhem, Mbagala wilayani Temeke, Dar es Salaam na mamia ya watu walijitokeza na kupimwa magonjwa mbalimbali yakiwamo maradhi ya moyo.

Katika upimaji huo, uliofanyika Alhamisi wiki hii, ikiwa sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, ambayo kilele chake ni kesho, watu 561 walipimwa viashiria vya magonjwa ya moyo na kati yao, asilimia 80 walikutwa na shinikizo la juu la damu huku asilimia 30 wakiwa hawajui kama wana tatizo hilo na kuanzishiwa matibabu.

Licha ya watu hao kubainika wana tatizo hilo, ilibainika kuwa asilimia 50 ya waliopimwa, walikuwa wanajua wana tatizo, lakini hawakuendelea na matibabu kutokana na sababu mbalimbali.

Hatua ya JKCI ya kuwafikia watu hao na kubaini matatizo hayo ni ya kupongezwa kwa sababu imeibua jambo ambalo huenda limewaamsha Watanzania wengi wakiwamo watunga sera na wale walioko katika ngazi za uamuzi, kwa maana ya viongozi.

Ni ukweli usiopingika kwamba Watanzania wanasumbhuliwa na matatizo mbalimbali licha ya kwamba hawajui kama wanayo. Hilo pia lilijidhihirisha wakati wa kampeni ya uchunguzi wa saratani ya matiti na ile ya shingo ya kizazi. Katika kampeni hiyo, wanawake wengi walibainika kuwa maradhi hayo, hivyo kuufanya umma kujua ukubwa wa tatizo hilo, hivyo hatua zinapaswa kuchukuliwa.


Kutokana na kuwapo kwa taarifa juu ya watu wengi kusumbuliwa na magonjwa ambayo ni viashiria vya maradhi ya moyo, ni vyema sasa hatua zikachukuliwa ili Watanzania wengi wafikiwe kwa kupatiwa elimu kisha upimaji wa hiari wa afya.

Kwa mtazamo chanya, ni vyema serikali ikatangaza kuwapo kwa kampeni mbalimbali za upimaji wa magonjwa mbalimbali katika ngazi za vijiji hadi mikoa kwa wataalamu wa afya kuwafikia wananchi katika maeneo yao.

Ni imani kwamba kwa kufanya hivyo, kuna uwezekano mkubwa wa kuokoa maisha ya watu wengi ambao watabainika kuwa katika hatua za awali za maradhi hayo na hatimaye kuwa na taifa lenye nguvu kazi yenye afya njema.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Hivi vinaweza kukwamisha somo la TEHAMA kwa shule za vijijini

**MWAKA** 2005, somo la teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) lilianzishwa katika mtalaa mpya wa elimu ya msingi na iliyokuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa lengo la kumpa mwanafunzi maarifa na stadi za matumizi ya habari, vyombo vya mawasiliano na maktaba.

Hatua hiyo inatokana na ukweli kwamba katika ulimwengu wa leo wa utandawazi, matumizi ya TEHAMA, hususani kompyuta, yamechangia maendeleo ya sayansi na teknolojia kuzidi kusambaa.

Hapa nchini, Kiswahili kinatumika kama lugha rasmi ya kufundishia somo hilo katika shule za msingi kama nyenzo ya kuwasilisha elimu ya sayansi na teknolojia ya kisasa kwa wanafunzi.

Pamoja na juhudi hizo za kuanzisha kwa somo hilo, bado kuna matatizo mbalimbali ambayo kwa namna moja ama nyingine, yanaweza kukwamisha ufundishaji na ujifunzaji wa TEHAMA.

Baadhi ya matatizo hayo, ambayo yamewahi kutajwa na wizara husika ni uhaba wa walimu, ukosefu wa umeme hususani maeneo ya vijijini na uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Kwa upande wa serikali, inajitahidi kutatua changamoto ya nishati kwa kupeleka umeme vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA), ili kuhakikisha somo hilo linafundishwa katika vyuo vya ualimu.

Lengo la kufanya hivyo, ni kuwaandaa walimu watakaofundisha somo hilo shuleni, huku ikishirikiana pia na kampuni ya Microsoft kwa ajili ya kupata vifaa hasa kompyuta.

Huo ni mpango wa muda mrefu wa serikali wa kuimarisha matumizi ya somo hilo katika ufundishaji shuleni, lakini bahati mbaya linafundishwa kwa baadhi ya shule, hasa za mijini zenye mazingira rafiki ikiwamo umeme.

Kwa mazingira hayo ni wazi kwamba, kuna umuhimu wa kuwaandaa walimu na pia kuhakikisha shule zote zinakuwa na umeme, ili iwe rahisi kwa walimu kufundisha na pia iwe rahisi kwa wanafunzi kuelewa.

Katika kitabu cha TEHAMA darasa la saba, kuna mada kama vile mtandao wa ndani wa kompyuta, mtandao wa intaneti, kutumia tovuti, maana ya baruapepe, hayo yote walimu na wanafunzi wanatakiwa kuyaelewa.

Sina uhakika kama walimu na wanafunzi wa shule za vijijini wanaweza kuyaelewa, ndiyo maana nikasema, kuna haja ya kuhakikisha shule zote zinakuwa na walimu wanaojua matumizi ya TEHAMA ili iwe rahisi kufundisha.

Itawawia rahisi walimu kufundisha iwapo pia shule zitakuwa na umeme kwa ajili ya kompyuta, hivyo ni vyema kasi ya umeme wa REA ikaongezeka ili kuhakikisha shule zote zinakuwa na nishati hiyo.

Shule za vijijini zisionekane kama zinabaguliwa kwenye somo la TEHAMA, kwa kuwa tu hazina nishati ya umeme, kwani huko nako kuna wataalam wa baadaye ambao wanahitaji kufundishwa somo hilo.

Hayo yakifanyika, wanafunzi wa shule za vijijini hawatakuwa nyuma kwenye somo hilo, hivyo umeme usambae kote, wizara husika iandae mafunzo ya muda mfupi kwa walimu wa vijijini ambao watafundisha TEHAMA.

Kama umeme wa REA unaweza kuchukua muda mrefu, basi uangaliwe uwezekano wa kuhakikisha shule zote zinakuwa na umeme wa sola ili kurahisisha ufundishaji wa somo hilo.

Siyo vibaya kushirikisha wadau wote wa elimu kwa ajili ya kufanikisha uwapo kwa somo hilo kwa shule zote nchini, kwani wanaweza kusaidia upatikanaji wa kompyuta mpakato, sola na huduma nyingine umuhimu.

Wakati hilo likifanyika, wizara husika nayo iwajengee walimu uwezo katika somo hilo, kutokana na mabadiliko ya teknolojia ya mawasiliano duniani, ambayo kimsingi huathiri nyanja mbalimbali za maisha.

Hayo yakifanyika, kutakuwa na mazingira rafiki ya ufundishaji na ujifunzaji wa somo hilo kwa shule zote nchini, bila kujali kwamba ni za vijijini au mijini, kwani kila moja itakuwa mahitaji yote muhimu.

Pamoja na hayo, ninaamini kwamba kuna manufaa mengi katika ufundishaji wa somo hilo kwa lugha ya Kiswahili, kwani inasaidia kujenga saikolojia ya kujiamini na kujithamini miongoni mwa wanafunzi.

Vilevile lugha ya Kiswahili ni hatua muhimu ya kukabiliana na mahitaji mapya katika medani za sayansi na teknolojia, tofauti na sura yake ya kuwa lugha ya kwenye majukwaa ya kisiasa, nyumbani na maeneo mengine.

SAFU

AFYA

# Maajabu ya tango katika kupambana na maradhi

Na Mwandishi Wetu

MATANGO yamekuwa maarufu kwa watu wengi kutokana kutumiwa kama chakula, juisi, tunda au saladi wakati wa mlo. Kila mtu hutumia kadri anavyoweza na namna anavyotengeneza wakati wa kuyatumia.

Wakati mwingine badhi ya watu huchanganya vuipande vya tango na vile vya ndimu au limau na kuchanganya na maji kisha kuweka kwenye chupa kwa saa kadhaa na kuanza kunywa. Wanaotumia hivyo husema wanakunywa ili kupungiza uzito.

Pamoja na sababu hiyo na kutumiwa kwa namna mbalimbali, huenda wengi hawajui faida zake. Lakini ukweli ni kwamba tango lina faida nyingi kiafya katika mwili wa binadamu.

Miongoni mwa faida hizo kiafya ni kama zifuatazo;-

**Kuondoa Sumu**

Kwa mujuibu wa wataalamu wa sayansi za afya, tango ambalo huwekwa katika jamii ya mboga na matunda, lina virutubisho muhimu kwa afya ya mwanadamu ikiwamo kuondoa sumu mwilini.

Kutokana na umuhimu huo, watu wanashauriwa kutumia tango ana liwe katika mfumo wa juisi kama baadhi wanavyotengeneza, kula likiwa bichi au kukatakata vipande na kisha kutafuna.

Kwa ujumla, kama yalivyo matunda mengine na mboga za aina mbalimbali, tango lina maji mengi ambayo humsaidia mtu ambaye mwilini ana sumu kutokana na kula vyakula, unywaji wa pombe na sumu za kimazingira, kuondokana na sumu hivyo kuwa na afya njema.

**Kuongeza Maji Mwilini**

Maji ni muhimu katika mwili wa binadamu. Kuwapo kwa maji mengi mwilini, huwezesha mmeng'enyo wa chakula kufanyika vizuri na pili kufanya joto kuwa katika hali nzuri.

Ulaji wa tango, husaidia mwili kuwa na maji yenye vitamini na viinilishe ambavyo huuwezesha mwili kuwa katika afya njema. Kwa mantiki hiyo, inashauriwa mtu kula tango mara kwa mara kwa ajili ya kufanya mwili kuwa na maji.

Kwa mujibu wa gazeti la afya ya 'Healthline', ulaji wa matunda na mboga huchangia asilimia 40 ya maji mwilini. Utafiti unaonyesha kuwa tango lina asilimia 96 ya maji huku asilimia zilizobaki zikiwa ni vitamin na viinilishe tu.

Faida za kuwa na maji mengi mwilini pia husaidia mtu kupata haja kubwa kwa urahisi na bila matatizo.

Kutokana na umuhimu huo, wanasayansi wanashauri kuwa wakati wa kiangazi, watu wanapaswa kula matango na matunda mengine kwa wingi ili kuwa na maji ya kutosha mwilini.

**Kupunguza Uzito**

Je, una uzito kuzidi mwili na urefu wako? Basi njia mojawapo ya kupunguza ni kula mboga na matunda kwa wingi .

Tango kama yalivyo matunda mengine na kama baadhi ya watu wanaovyodhani kuwa ni jamii ya mboga,



ina virutubisho vingi ambavyo husaidia kupunguza uzito katika mwili. Hiyo ni kutokana na kuwa na 'kalori' chache.

**Kupambana na sukari**

Utafiti wa kisayansi unaonyesha kuwa mtu mwenye tatizo la sukari mwilini, anakuwa katika nafasi nzuri ya kupunguza ugonjwa huo na kudhibiti tatizo kuwa kubwa.

Katika moja ya utafiti uliofanywa, kwa mujibu wa Healthline, ulaji wa tango mara kwa mara unasaidia kupunguza tatizo la sukari kwa mgonjwa. Utafiti huo ulihusisha panya ambaye aliwekewa sukari na kupewa matango. Baada ya muda Fulani, sukari katika mwili wa panya huyo ilipungua kwa kiasi kikubwa.

**Shinikizo la Damu**

Tango ni chanzo cha madini ya potasiamu, magnesiamu pamoja na nyuzinyuzi. Vitu hivyo ni virutubisho muhimu katika kupambana na shinikizo la damu katika mwili wa binadamu.

Utafiti unaonyesha kuwa utumiaji wa mara kwa mara wa tango hasa juisi yake, husaidia kupunguza tatizo la shinikizo la damu hasa lwa wazee ambao tayari wanasumbuliwa na maradhi hayo.

**Kuimarisha Ngozi**

Utumiaji wa mara kwa mara wa tango husaidia ngozi kuwa nyororo na yenye afya. Hiyo ni kutokana na virutubisho ambavyo huifanya ngozi kutokutoka jasho kwa wingi.

Sambamba na hiyo, unywaji wa juisi ya tango husaidia ngozi kuwa ng'avu wakati wote na kupunguza vipele na muwasho. Kwa ujumla, ulaji wa tango mara kwa mara una faida nyingi kwa mwili wa binadamu. Miongoni mwa manufaa hayo ni kupunguza uzito wa mwili, kuwa na uwiano mzuri wa maji mwilini, mfumo wa chakula kuwa bora na kupungua kwa kiwango cha sukari mwilini.

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Tunahitaji sauti moja kukabiliana na nimonia



Na Joseph Kulangwa

Juhudi za Rais John Magufuli kujenga hospitali, zahanati na vituo vya afya nchi nzima, zikisimamiwa na Waziri wa TAMISEMI, Selemani Jafo, zinafunikwa na sauti ya nyungu.

DUNIA inapitia kipindi kigumu sana kiafya kwa sasa. Wakati ikipambana na ugonjwa wa COVID -19, sisi Tanzania tunapamba na nimonia ambayo inaonekana kutuathiri vibaya kimaisha.

mwaka jana, Tanzania tulipambana sana na COVID-19 lakini kwa maombi yaliyosikika na Mwenyezi Mungu tuliitokomeza na kuishi maisha tofauti na mataifa mengine, ambayo yaliendelea kuteseka.

Lakini wakati mataifa hayo mwaka huu yakilalamika kukumbana na aina mpya ya virusi vya korona, sisi tukajikuta tunaingia katika wimbi la maambukizi ya nimonia, ambayo inasababisha changamoto za upumuaji.

Nimonia hii imetupokonya wapendwa wetu, huku dalili zake zikifanana kabisa na za COVID-19 na mbinu zake za kujikinga zikifanana pia, katika kuvaa barakoa, kutumia vitakatishi, kunawa maji tiririka na sabuni na kujiepusha na misongamano.

Inaonekana kila mwaka kutakuwa na ugonjwa mpya kwani baada ya Corona sasa tuna nimonia, hatujui mwaka ujao tutakuwa na ugonjwa gani.

Baadhi ya wataalamu wanasema nimonia hii inatokana na mabadiliko ya hali ya hewa, ambayo hutokea nyakati hizi kila mwaka.

Lakini kinachoonekana ni tofauti, kuwa nimonia ya miaka iliyopita haikuwa kali kama hii ya mwaka huu na kushabihiana na Corona, ndiyo sababu hata baadhi ya watu wakiwamo wanasiasa, hawataki kabisa nimonia hii iitwe Corona, kwa sababu ni magonjwa tofauti, ingawa yanashabihiana.

Hata baadhi ya wataalamu wetu wa tiba nao wanamsimamo huo, hivyo Watanzania kukosa budi kuwaamini kwa kuwa katika fani hiyo, wao ndio Alfa na Omega. Bora waachwe waendelee kupambana na nimonia mpaka tuitokomeze kama tulivyofanikiwa kwenye Corona.

Pengine tofauti na mwaka jana kwenye mapambano dhidi ya COVID-19, mwaka huu dhidi ya Nimonia, karibu kila mtu anapambana kivyake. Imekosekana sauti ya pamoja kama tulivyozoea Watanzania katika kuhamasisha mapambano. Rejea mwaka jana kwenye Corona, rejea miaka ya sabini kwenye Vita vya Kagera.

Leo kwenye nimonia, kila mtu anasema lake, kila mtu anashauri lake, waganga wa jadi ni wengi, wataalamu wa tiba ni wengi, dawa za kukabiliana na Nimonia ni nyingi tena za aina mbalimbali, kila taasisi ina dawa yake, fomula na bei yake.

Wakati wataalamu wa tiba wanakuja na dawa za kisasa, wa asili wameshikilia nyungu-kujifukiza; wanasiasa nao wamekumbatia nyungu, kiasi kwamba wapo wanaopendekeza kila hospitali iwe na chumba maalumu cha kujifukizia.

Wakati hilo likiendelea, baadhi ya wataalamu wanasema kujifukiza kuna athari mbaya kwenye mapafu, lakini waliojifukiza wanasema nyungu imewaondolea nimonia.

Juhudi za Rais John Magufuli kujenga hospitali, zahanati na vituo vya afya nchi nzima, zikisimamiwa na Waziri wa TAMISEMI, Selemani Jafo, zinafunikwa na sauti ya nyungu. Watu wanahamia kwenye nyungu na kuacha vituo vya afya!

Ukweli ni kwamba miluzi inaanza kumpoteza mbwa. Tangawizi, limao, vitunguu, pilipili kichaa na asali, vinaanza kufunika dawa za hospitali, vinafunika mashine za kusaidia kupumua. Wangapi wanapona, Mungu ndiye anajua.

Pamoja na yote hayo, na imani zote hizo, na mikanganyiko yote hiyo, bado ipo haja ya kuwa na sauti moja katika kukabiliana na matatizo. Ugonjwa uliopo bila kujali unaitwaje, unatakiwa kuchunguzwa na kuja na njia moja ya kuukabili kwa maslahi mapana ya afya ya jamii.

Tukishindwa katika nimonia ya mwaka huu, je, hiyo ya mwakani itakayoibuka kipindi kama hiki kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa, tutafanya nini katika kuikabili?

**Alamsiki!**

## KONA YA UKWELI

# Watendaji serikalini mmemsikia JPM, urasimu utoaji habari basi



Na Thobias Mwanakatwe

**Tatizo hili ambalo limekuwa la muda mrefu, linasababisha waandishi na vyombo vya habari kushindwa kupata taarifa kutoka serikalini ili wananchi wafahamu nini kinachoendelea katika serikali yao.**

SEKTA ya habari ni moja ya sekta za huduma za jamii nchini. Sekta hii inatoa huduma ambayo ni haki ya msingi ya raia kama inavyotamkwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Katika Ibara ya 18 ya Katiba hiyo inasema: "Kila raia anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali nchini na duniani kote ambayo ni muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia juu ya masuala muhimu kwa jamii."

Aidha, kutoa na kupokea habari kunatambuliwa duniani kote kuwa ni moja ya haki za binadamu. Umoja wa Mataifa, na Umoja wa Afrika zina matamko rasmi ambayo serikali imeridhia kuhusu haki ya kupokea na kutoa habari.

Haki hii, kama zilivyo haki zingine, hutolewa kwa kuzingatia wajibu wa kila raia kwa jamii na uhuru binafsi wa binadamu.

Dhima ya sekta ya habari na utangazaji katika jamii ni kutoa habari, kuelimisha na kuburudisha. Sekta hii inahudumiwa na vyombo vya habari ambavyo ni redio, magazeti, majarida, televisheni, filamu, video, intaneti na kadhalika.

Pamoja na umuhimu wa sekta hii, hapa nchini kumekuwa na tatizo katika baadhi ya ofisi za serikali zikiwamo wizara taasisi na idara watendaji na viongozi wa serikali kutotoa ushirikiano wa kutoa taarifa kwa vyombo vya habari.

Tatizo hili ambalo limekuwa la muda mrefu, linasababisha waandishi na vyombo vya habari kushindwa kupata taarifa kutoka serikalini ili wananchi wafahamu nini kinachoendelea katika serikali yao.

Kinachoshangaza watendaji wa serikali wanaoficha habari hawana sababu za msingi badala yake baadhi yao wanaficha madhambi mengi wanayoyatenda katika ofisi wanazoziongoza.

Nampongeza Rais John Magufuli kwa kubaini kuwapo kwa urasimu katika utoaji habari unaofanywa na baadhi ya watendaji.

Rais Magufuli Februari 25, mwaka huu, akizindua studio ya televisheni ya Channel 10 na Magic FM mkoani Dar es Salaam ambavyo vinamilikiwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM), aliwataka watendaji wa serikali kuwa wepesi kwenye kutoa taarifa kwa sababu ziko baadhi ya wizara na taasisi za umma ambako waandishi wakienda kufuata taarifa habari zinafichwa bila sababu ya msingi.

Rais Magufuli alisema serikali yake haiogopi kupewa changamoto wala kukosolewa kama kukoselewa kwa staha. Akasema katika kipindi cha miaka mitano serikali yake imeruhusu vyombo vingi zaidi vya habari kuliko wakati mwingine wowote tangu taifa hilo lipate uhuru.

Alisema mwaka 2015, Tanzania ilikuwa na vituo vya redio 106 na televisheni 25 lakini hadi kufikia februari, mwaka huu, kuna ya vituo vya redio 193, televisheni 46, magazeti 247, televisheni za mtandao 443 na redio za mtandao 23.

Licha ya ongezeko hilo, Rais Magufuli, aliwataka waandishi wa habari kuweka mbele uzalendo na maslahi ya taifa kwanza na kufanya kazi kwa kuzingatia haki hasa kwa yule ambaye habari inamhusu. Pia aliongeza kuwa kumekuwa na habari nyingi za uzushi zingine zikizushia watu vifo wakiwemo viongozi na watu mashuhuri.

Kauli kama hii ya urasimu kwa baadhi ya watendaji serikalini ilishawahi kutolewa pia na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa Machi 18, 2019 wakati akifungua kikao kazi cha maofisa mawasiliano wa serikali kilichofanyika jijini Mwanza.

Majaliwa alisema kuna baadhi ya watendaji na viongozi wa Serikali ambao wana urasimu katika utoaji wa habari na kuwataka waache mara moja.

Alisema Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 inawataka watendaji kutoa taarifa kwa umma ambazo zinatakiwa kutolewa, lakini bado baadhi yao wanaendelea kuzikumbatia.

"Wapo baadhi ya watendaji bado wanatumia urasimu kutoa taarifa, jambo hili halikubaliki hata kidogo, lazima taarifa zinazotakiwa kutolewa kwa umma zitolewe," alisema.

Kauli hizi za viongozi wa juu wa serikali, watendaji na viongozi serikali mnaposhindwa kuzifanyia kazi kwa vitendo tafsri yake ni kwamba mnadharau wakubwa wenu.

Watendaji serikalini ni lazima mtambue kuwa mnapoficha taarifa hamvikomoi vyombo vya habari bali mnavunja katiba kwa kuwanyima haki wananchi ambao katiba inawapa haki ya kupata habari.

Ni matumaini kuwa baada ya tamko hilo la Rais Magufuli mtabadilika na kutoa ushirikiano kwa vyombo vya habari ili kutimiza matakwa ya katiba.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA**

**Kwa maoni na ushauri tumia ujumbe au nipigie kwa 0762-183666**

## DARASA LA NDOA

# Umuhimu wa wazazi kuwa karibu na watoto



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka 0744000066

NYUMBA ni mahali pa malezi na kutoa mafunzo ya maadili na mwenendo mwema kupitia mfano na mafundisho ya wazazi. Nyumba si jengo tu watu wanamokaa, bali ni mahali pa faraja, starehe na kushiriki amani na furaha.

Kwa maana hiyo, wazazi wanaotimiza wajibu wao wa malezi mema kwa watoto, wanajenga kizazi cha baraka katika familia na jamii. Kinyume na hapo, nyumba huweza kuwa uwanja wa fujo na chanzo cha laana na mikosi.

Matatizo mengi yanayotokea leo katika ndoa, familia na jamii kwa ujumla, hutokana na malezi mabaya wakati wa utoto, hali iliyoathiri makuzi. Watu wengi wameharibika kutokana na uzoefu mbaya kutoka kwa wazazi wao.

Mfano, baba au mama alikuwa hatimizi majukumu yake katika familia; haonekani nyumbani na wala haimsumbui kutokuonekana nyumbani; hana muda na watoto wake na mke/mume wake. Wengine wana uzoefu kutoka kwa wazazi wao wa vitendo vya ukatili, unyanyasaji, ulevi, wizi, kutukana, kutokujali, maisha ya amri, uvivu, kutelekeza na kadhalika.

Hawajawahi kuona matendo ya upendo ya baba au mama yao. Wazazi wamekosa kuwa kielelezo kizuri kwa watoto wao. Matokeo yake watoto hawa wakiwa watu wazima, kuna uwezekano mkubwa wa wao kufanya vivyo hivyo, kwani ndicho walichokiona na kujifunza kutoka kwa baba au mama yao. Wanakuwa watu waliotengenezwa kuwa hivyo.

Familia ni taasisi ya kuadabisha. Ni shule ya kwanza ya mafunzo kwa watoto, ambamo raia wema, waumini, viongozi, waume na wake bora hutengenezwa. Malezi na makuzi mazuri ya watoto yanategemea sana ukaribu wa wazazi kwa watoto wao. Kuwa karibu na watoto na kufuatilia maendeleo yao ni muhimu. Ni rahisi sana kubadili au kurekebisha kitu kwenye umri wa utoto kuliko akiwa mtu mzima.

Familia ndiyo msingi wa maadili mema kwani tabia na mienendo yetu inajengwa katika familia. Maadili ya viongozi yanajengwa kuanzia katika ngazi ya familia. Ili tuwe na viongozi bora na waadilifu, lazima mkazo uwekwe katika malezi ngazi ya familia.

Maendeleo yanahitaji watu waadilifu. Uadilifu huo huanza kujengwa katika familia. Haya yote yatawezekana pale wazazi watakapotimiza ipasavyo wajibu wao wa malezi na kujenga ukaribu na watoto.

### Umuhimu wa kuwa karibu na watoto

Muda anaotumia mzazi pamoja na watoto wake ni muhimu sana katika makuzi yao. Ukaribu wa wazazi unasaidia yafuatayo:

- Kuwafahamu vizuri watoto na watoto nao kuwafahamu wazazi wao vizuri (tabia, hisia zao,vipawa vyao, matamanio yao, n.k).
- Kutambua changamoto na mahitaji yao muhimu kwa kuwapa fursa ya kueleza na kusikilizwa.
- Kubadili mitazamo yetu juu yao. Wakati mwingine wazazi tunakuwa na mitazamo chanya au hasi kuhusu watoto wetu kwa sababu ya kutokuwafahamu vizuri.
- Ni njia ya mzazi kuonesha kuwa anajali na kuwapenda watoto wake. Watoto wanapojua kuwa wanapendwa, wanajengewa msingi imara wa kujali na kupenda watu wengine pia.

Ukaribu huu unaimarisha mawasiliano kati ya mtoto na mzazi. Ni muhimu wazazi kuwa na mawasiliano mazuri na watoto hasa wanapokuwa na umri wa kuanzia miaka 13. Katika umri huu watoto hujijengea imani halisi. Watoto wanakuwa na hali ya kujaribu mambo na mara nyingi hufanya uchaguzi usio sahihi kadri wanavyokua.

Ni muhimu wazazi kupanga muda wa kuwa na watoto mara kwa mara. Muda mzazi anaotoa kwa ajili ya watoto/mtoto wake ni wa thamani sana na utasaidia kujenga uhusiano mwema kati ya mzazi na mtoto kwa maisha ya leo na hapo baadaye.

Ili kutekeleza jukumu hili vizuri ni muhimu wazazi kujua namna ya kutawala muda wao. Ifahamike kuwa, wako watoto ambao wamewachukia wazazi wao (baba au mama) na kazi wanazozifanya. Watoto wamepoteza tumaini la maisha kwa sababu ya kuhisi kutelekezwa na wazazi wao.

Wazazi wote wana shughuli nyingi ndiyo maana ni muhimu kwa wazazi kuhakikisha ya kuwa wanapanga muda wa kuwa na watoto wao. Kwa kufanya hivyo, mzazi anakuwa anamwonesha mtoto wake kuwa, licha ya shughuli nyingi alizonazo, mtoto/watoto wake ni kipaumbele chake.

Kila mzazi atavuna alichopanda kwa mtoto wake. Ukipanda mema, utavuna mema na ukipanda mabaya, utavuna mabaya. Inawezekana athari usizione leo, bali hapo baadaye. Watoto waliolelewa vibaya hawako salama sana, kwani dhamiri zao zinakuwa butu kukabiliana na changamoto na mazingira tofauti. Wazazi wenye malezi bora huwakuza watoto katika hali salama, ambayo itawawezesha kujisimamia katika maisha yao.

Wakati mwingine wazazi tumewakosea watoto wetu kwa kuwalaumu na kuwalaani kwa makosa yetu wenyewe.

Ni muhimu mzazi kuangalia mahali ulipokosea na kuanguka. Badala ya kuwa mkali kwa watoto wako, uwe mpole tu, zaidi sana waombe msamaha watoto wako kwani inawezekana wewe mwenyewe ndio chanzo cha hayo unayokutana nayo leo kutoka kwa watoto wako. Yajenge na watoto wako ili maisha yawe salama na yenye amani.

Wazazi wenye ufahamu na kujali watahakikisha wanaruhusu watoto wao kujifunza mambo mema kutoka kwao.

Hii inakuwa ni hazina njema hasa pale wazazi wanapofikia ukomo wa maisha yao ya hapa duniani, watoto wanabaki na hazina ya maarifa na ufahamu vitakavyowasaidia kuishi maisha ya utulivu, ushindi na mafanikio.

Kwa hiyo, ni muhimu wazazi wajifunze kuwekeza malezi bora kwa watoto wao ili kuepuka maumivu na majuto leo na hapo baadaye.

# MAISHA

Machi 7, 2021

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




Ndugu, jamaa na marafiki wa familia ya Mbago, wakiwa na furaha wakati wa sherehe ya kumuaga binti yao kipenzi, Judith Februari 28, mkoani Tanga.

## HARUSI

Ukurasa 12



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

PAZIA kupendezesha nyumba

## Mkate wa mayai

Ukurasa 14





# PAMBA ZA MASIKIO

## Ni hatari kusafishia, wengi kuwa viziwi

Ukurasa 14

# Tumewachanganya, wamechanganyikiwa hasa!

**Na Moses Ismail**

NI kweli ni msichana wa miaka kumi na zaidi, bado hajafikisha miaka kumi na tisa, lakini 'mambo yake' ni tofauti na binti wa umri wake.
Ukimuita, 'anakukata jicho' kisha anaendelea na safari zake bila ya kujali tofauti ya umri kati yenu. Jaribu sasa kusisitiza kumuita kama unavyomchukulia, kuwa ni binti mdogo tu, utasikia akikujibu"
"We baba vipi. Wanawake wa saizi yako hujawaona?"
Kwa vile hukumita wala kumuangalia kama 'mwanamke', majibu yake yanakushangaza, unabaki umeduwaa tu na ndipo unapomtazama na kugundua kuwa hata mavazi na mikogo yake ni kama ya wasichana wakubwa wa miaka 18. Kana mambo yaliyotangulia umri wake!
Hii ni jambo la kawaida kwa mabinti wa mijini, ingawa hata na vijijini pia wapo. Kwamba katika umri mdogo tu akili zao zimeshawafunulia hisia za kujiona wao ni 'wanawake hasa' na kila mwanamume anawangalia kama 'wanawake'.
Kwa kulijua hilo, ndipo unapojiuliza ni wapi wasichana hawa wamepata hisia hizi za kuwa kila mwanamume anayemwita barabarani anamtaka kimapenzi?
"Wanapata wapi?!" anauliza kwa mshangao Hilda Juakiko, mkazi wa Sinza jijini Dar es Salaam, kisha naye anauliza: "Hivi na haya mabazazi yanayofuata fuata wasichana wadogo ina maana hamyaoni au vipi?".
Juakiko anasema; "hao mabazazi ndio wanaofanya wajenge hisia kuwa kila mwanamume anawaita anataka kuwatongoza, kwa sababu kila mara wanakutana nao barabarani na kazi yao ni hiyo hiyo tu."
Ni kweli, wapo wanaume mabazazi kama anavyoyowaita Juakiko, lakini hiyo tu ndiyo sababu ya pekee katika tatizo hili?

Simon Bangu, mwanasaikolojoa mkazi wa Dar es Salaam anatoa majibu ya jumla kwa maswali kadhaa juu ya jambo hilo akiliangalia kwa muktadha wa kisaikolojia zaidi. Anasema:
"Unajua msichana mpaka anapojiona kuwa yeye sasa ni 'mwanamke' si jambo linalozuka tu, bali ni jambo linalojengwa kiakili na mambo mengine yanayoijenga akili yake kujiona hivyo yanaonekana ni madogo sana lakini yanaathari kubwa sana.
"Kwa mfano tabia ya wazazi wanawake, mashangazi, mabibi, mama wadogo na madada ya kupenda kuwasifu watoto wa kike kwa uzuri wao tangu wakiwa wadogo nayo inamjenga mtoto kujiona ana thamani fulani mbele za mwanamume.
"Hii ni kwa sababu sifa nyingi anazopewa mtoto wakike zinalenga kumuonyesha kuwa atapendwa na wanaume. Utasikia anaambiwa; 'kwa shepu yako, wanaume lazima wauane'. Hilo ni tatizo kubwa na baya sana kimalezi.
"Na hili si kwa wasichana wazuri tu, hata wale ambao wanabezwa kwa 'ubaya', ambao kila mara wanaambiwa 'wewe sijui kama utapata mwanamume wa kukuoa'. Hawa huingia katika mkumbo huo ili wajithibitishie tu kama na wao wanawavutia wanaume na hilo hulifanya kwa kuwajaribu wanaume".
Inawezekana kuwa tatizo katika suala hili ni la wazazi au 'mafataki, kwamba wao ndio wanaowaongoza mabinti kuwa hivyo. La msingi ni kwa jamii kurejea katika mstari na kusaidia kuondoa hali hii kila mmoja kwa nafasi yake.

## NA HAMIS KIDAGO

0657 207168

# QUIZ

### LE QUIZ DU WEEK

Le Verbe Suivre – Kitenzi "Fuata"

1. Kamilisha unyumbuaji wa kitenzi "Fuata" katika nyakati mbalimbali kama zilivyoainishwa hapo chini.


Indicatif
present
je ..............................
tu ..............................
il/elle ..............................
nous ..............................
vous ..............................
ils/elles ..............................
imparfait
je ..............................
tu ..............................
il/elle ..............................
nous ..............................
vous ..............................
ils/elles ..............................
futur simple
je ..............................
tu ..............................
il/elle ..............................
nous ..............................
vous ..............................
ils/elles ..............................
passé simple
je ..............................
tu ..............................
il/elle ..............................
nous ..............................
vous ..............................
ils/elles ..............................
passé compose
j' ai ..............................
tu as ..............................
il/elle a ..............................
nous avons ..............................
vous avez ..............................
ils/elles ont ..............................
plus – que – parfait
j' avais ..............................
tu avais ..............................
il/elle avait ..............................
nous avions ..............................
vous aviez ..............................
ils/elles avaient ..............................
futur anterieur
j' aurai ..............................
tu auras ..............................
il/elle aura ..............................
nous aurons ..............................
vous aurez ..............................
ils/elles auront ..............................
passé anterieur
j' eus ..............................
tu eus ..............................
il/elle eut ..............................
nous eumes ..............................
vous eutes ..............................
ils/elles eurent ..............................
Conditionnel
present
je ..............................
tu ..............................
il/elle ..............................
nous ..............................
vous ..............................
ils/elles ..............................
passé
j' aurais ..............................
tu aurais ..............................
il/elle aurait ..............................
nous aurions ..............................
vous auriez ..............................
ils/elles auraient ..............................
Infinitif
present
..............................
passé
..............................
Participe
present
..............................
passé
................/..............
................/..............
..............................
Imperatif
present
..............................
..............................
..............................
passé
..............................
ayons ..............................
..............................
Subjonctif
present
que je ..............................
que tu ..............................
qu' il/elle ..............................
que nous ..............................
que vous ..............................
qu' ils/elles ..............................

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA KIDOGO



**Popo yupo katika kundi gani la wanyama?**

**WANAFUNZI walikuwa wanafanya mitihani yao ya maarifa, katika majibu yao hawakutakiwa kufuta au kukata kwa peni.**
**Swali la kwanza,**
**Taja vyakula vitatu ambavyo ukienda hotelini na umelipiwa utapenda kula?**
**Wavulana wakajaza; wali, ugali na mihogo.**
**Wasichana wakajaza; burger, pizza, egg chop.**
**Swali la pili**
**Eleza jinsi ya kupika kila chakula ulichotaja hapo juu. (alama 99)**
**Wafulana walijibu kwa haraka, lakini wasichana walitazamana na hawakuweza kufuta majibu ya mwanzo.**

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Waliokusingizia wataona aibu mbele ya macho yako

KARIBU tena msomaji wangu katika safu yetu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo. Leo tusikie ushuhuda wa roho ya kusingiziwa inavyoweza kumuinua aliyeteswa.
Ni roho ambayo imetesa maisha ya watu wengi, wengine wakiuawa na kufungwa magerezani.
Hujafanya jambo lolote lisilopendeza lakini unasingiziwa kulifanya, siyo mchawi unaambiwa umemloga fulani. Hujaiba unaitwa mwizi. Hii ni roho ya kusingiziwa tunaishi nayo katika maisha yetu ya kila siku. Ni roho ya kulazimishwa kuhusika wakati siyo kweli.
Mifano ya watu kusingiziwa jambo ni mingi na tumeishuhudia katika maisha. Wengi wametaabika sana lakini kwa kuwa Mungu ni kweli na uzima, pia mwenye haki, amewaumbua wasingiziaji, tena mbele ya macho yao, wakabaki wanashangaa!
Hebu msomaji wangu fuatana na kisa hiki uone mkono wa Mungu unavyookoa watu mbele ya maadui zao. Mama mmoja huko Tarime, mkoani Mara, alifiwa na mumewe na kumuachia watoto 13, wa kike saba na wa kiume sita.
Kabla ya mumewe kufariki walikuwa wamejenga nyumba mbili nzuri, walikuwa na gari, mashamba na wamiliki wa mifugo. Mara tu baada ya mazishi, ndugu wa mume wakamnyang'anya mali zake zote alizochuma na mumewe na kumuacha bila kitu isipokuwa watoto wake.
Ndugu hao walimtuhumu mjane huyo kwamba ndiye aliyehusika na kifo cha mumewe kutokana na kwamba alianguka bafuni ghafla na kufa papo hapo. Wakati huo mtoto wa kwanza alikuwa binti wa miaka 17 na wa mwisho wa kiume umri miezi tisa.
Wakati wanafukuzwa kwenye nyumba yao na kunyang'anywa mali zote, mama aliwakusanya watoto wake na kuanza kuishi mitaani kama ombaomba. Watoto walishindwa kuendelea na shule kutokana na kukosa ada na kuanza kuokota vyakula majalalani. Ulikuwa ni wakati mgumu kwa mama na watoto wake kwani hawakuwahi kuishi maisha mabaya kama hayo.
Isitoshe, kitendo cha mama kutuhumiwa kuwa yeye ndiye aliyehusika kumuua mumewe, kilimfanya achanganyikiwe.
Kwa muda wa miaka mitatu hali ilikuwa mbaya sana.
Binti yake pamoja na wadogo zake wakaanza kujitambua na kufanya kazi ndogo ndogo kwenye mashamba ya watu ili wapate chakula. Wakati huo mama yao alikuwa hajatulia.
Baada ya sintofahamu hiyo ya maisha hayo la kulala njaa na kutangatanga mitaani, walifanikiwa kupanga nyumba yenye chumba na sebule baada ya miaka mitatu ya mateso, dhihaka, matusi ya kila aina.
Haikuishia hapo, baada ya kupata makazi kujistiri, mjane akili ilimrejea. Akapata wazo la kufanya kazi yoyote ya mikono kwenye nyumba za watu au ofisini ili ajipatie kipato cha kuishi wanawe.
Alifanya kazi kwa bidii akaanza kurejesha wanawe shule mmoja baada ya mwingine.
Siku moja akiwa katika shughuli zake, alikutana na dada mmoja mfanyakazi kwenye mashirika ya Utalii, Serengeti.
Yule dada akatokea kumpenda kutokana na bidii yake ya kazi, uaminifu na utendaji wake wa kazi akaamua kumuajiri msimamizi wa nyumba yake.
Yule mama aliendelea kufanya kazi kwa yule dada kwa uaminifu mkubwa na kwa kumheshimu ijapokuwa mjane alikuwa na umri mkubwa. Baada ya kuona utendaji kazi wake, yule dada alimuunganisha na wazungu waliokuwa wakitalii katika mbuga za wanyama za Serengeti kama mpishi.
Kitendo hicho cha kuunganishwa na wazungu, kikawa ndiyo chanzo historia yake kubadilika. Wale wazungu walitokea kumpenda sana na kumheshimu. Walifuatilia historia yake na kugundua kuwa alikuwa na watoto 13 na kwamba alitelekezwa na ndugu za marehemu mumewe.
Wale wazungu waliamua kufadhili masomo watoto wote na mama yao pia . Baada ya miaka kadhaa walimchukua yule mama na watoto wake na kuwapeleka nchi za ulaya kwenda kufanya kazi.
Hadi sasa inapotolewa simulizi hii, watoto wa kike wameolewa na wazungu na baadhi wa kiume wameoa wazungu na maisha yao ni mazuri kuliko mwanzo.

**Hakika Maisha Ndivyo Yalivyo.Nataka nikuambie msomaji wangu, haijalishi ni mara ngapi utaanguka fahamu ya kwamba utainuka tena. Bila shaka, msomaji umejifunza kitu hapo. Tukutana wiki ijayo. Una maoni, kisa cha kimaisha? Tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581.**

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Usafiri wa mabasi kituo kipya uangaliwe kwa jicho la pekee

KITUO Kikuu cha Mabasi cha Magufuli cha Mbezi Luis, kimeanza kufanya kazi na sasa huduma zote za usafiri wa mikoani zinaanzia na kumalizikia eneo hilo.
Kituo hicho ni cha ubora wa juu Tanzania kwa kuwa kimejengwa kisasa na hadi siku kinafunguliwa rasmi, kilikuwa na miundombinu ya awamu, huku jitihada zikiendelea kukamilisha miundombinu ya msingi ya watumiaji wengine ikiwamo barabara ya kuingia na kutoka kituoni humo.
Kutokana na upya wake, bado kuna changamoto nyingi hasa kutokana na miundombinu mingine kutokamilika ipasavyo, na inaendelea kutengenezwa ili kuhakikisha watumiaji wote.
Tatizo kubwa lililopo kwa sasa ni ongezeko la wapigadebe waliohama kutoka kituo kikuu cha zamani cha mabasi cha Ubungo na kwenda eneo hilo, huku ikionekana imekuwa ngumu kuwadhibiti.
Nyingine ni utaratibu wa kuwafikisha abiria wote ndani ya kituo hicho huku baadhi ya njia wakiacha kushusha abiria njiani, jambo ambalo ni usumbufu sana.
Mathalani, msafiri kutoka mikoa ya Kusini yaani Mtwara na Lindi, anatakiwa kushuka Mbagala na Temeke pekee zaidi ha hapo haruhusiwi kwa kuwa hakuna vituo rasmi vya magari ya mikoani kushusha abiria.
Mfano abiria anayeshuka TAZARA, Buguruni, Tabata au Ubungo anatakiwa kwenda hadi Mbezi ndiyo atafute utaratibu wa kurudi nyumbani kwake, jambo ambalo ni usumbufu mkubwa kwa kupoteza muda bila sababu.
Ninawaza kuna sababu gani ya abiria kupoteza muda wakati ungewekwa utaratibu angeshuka eneo analotakiwa kushuka kwa urahisi zaidi, na kuondoa mkusanyiko wa watu katika eneo la Mbezi.
Utaratibu huo unajitokeza kwa magari yanayotumia njia ya Bagamoyo, ambayo hupita njia ya Goba na hairuhusiwi kushuka, na abiria analazimika kwenda Mbezi ndiyo afanye utaratibu wa kurudi nyumbani kwake.
Naamini mamlaka husika zitaona tatizo hilo na kuja na suluhisho ya kudumu la kuondoa usumbufu kwa kuwa na vituo maaluma, mathalani Buruguruni, Tabata na Ubungo.
Kama iliwezekana kwa njia ya Morogoro maana yake utaratibu huo huo utumike kwa njia nyingine, ili kupunguza usumbufu ambao siyo wa lazima kwa wasafiri.
Pia ni muhimu kuwapunguzia gharama ya muda na fedha wasafiri hao, kwa kuwa inawezekana kuokoa fedha hizo kwa kushuka kituoni na kuzitumia katika shughuli zingine za maendeleo.

Ni muhimu sana ukafanyika utaratibu wa kuhakikisha ustaarabu na maana ya kituo hicho, vinginevyo kitachafuka, kitaharibika na kupoteza ubora amabo umetengenezwa kwa mabilioni ya fedha.
Tatizo jingine ni mabasi yote kulazimishwa kuanza na kumaliza safari zake kituoni humo, kwamba anayeishi Kigamboni hata kama gari awali lilikuwa na ofisi eneo hilo ni lazima aje kwa usafiri mwingine hadi Mbezi.
Pia mabasi mengi yalikuwa na ofisi eneo la Shekilango lakini tangu kuanza ka kituo hicho, wanatakiwa kuhamia Mbezi, jambo ambalo litaongeza songamano na usumbufu wakati ingewezekana kuweka utaratibu wa kulipa ushuru wote muhimu lakini waanzie kwenye ofisi zao na baadaye kuingia kituoni humo kuchukua abiria wengine.
Ni matarajio kuwa miundombinu muhimu kama barabara ya juu kutoka upande mmoja kwenda na kutoka kituoni humo itakamilika kwa haraka.

Aidha, bado kasi ya ujenzi wa miundombinu muhimu ya mama lishe na baba lishe, ili kuwaondolea adha ya kupika au kufanya shughuli zao kwenye eneo la wazi na lenye jua kali ambalo si sahihi kwa afya zao.
Iwapo miundombinu hiyo itakamilika kwa wakati kutasaidia sana mpangilio wa utumiaji, ikiwamo kurahisisha utoaji wa huduma zote muhimu kama choo na nyingine.
Ni muhimu watoa huduma za usafiri wa Bajaji na pikipiki ambao kwa sasa wanaegesha eneo la nje ambalo ndilo lango la mabasi kuingia, jambo ambalo ni hatari kwa watumiaji.
Iwapo kutakuwa na utaratibu wa kuegesha vyombo hivyo vya usafiri ili kuendeleza ustaarabu ambao ni muhiu katika kutunza hadhi ya kituo hicho, bila kufanya hivyo ni sawa na kwamba kituo hicho hakina utaratibu maalum wa waliostaarabika.
Pia ni muhimu kukamilisha kwa ukamilifu barabara za kuingia na kutoka, ili kupunguza msongamano nyakati za asubuhi na jioni.



Ndugu, jamaa na marafiki wa familia ya Mbago, wakiwa na furaha wakati wa sherehe ya kumuaga binti yao kipenzi, Judith Februari 28, mkoani Tanga.







# MITINDO



# UMEALIKWA HARUSINI?

## BASI ZINGATIA HAYA KABLA HUJAHUDHURIA

MWAKA 2021 umeanza na shamrashamra nyingi, kila kukicha mitaa mbalimbali inapambwa na sherehe za kila namna.
Mialiko imekuwa jambo la kawaida kiasi cha watu kuwa na kadi ya zaidi ya moja, zote zikiwataka kuhudhuria katika shughuli zao bila kukosa.
Kutokana na umuhimu wa shughuli hizo za kijamii, leo nitawapa miongozi ya nini cha kufanya wakati unapoalikwa kwenda katika sherehe ya harusi ili uwe na mwonekano mzuri.
Si jambo zuri kukuacha uhuthurie harusi ukiwa na mavazi yaliyopitwa na wakati au kukupotezea mvuto.
Pale unapoalikwa katika harusi, kuna mambo matatu ambayo hautakiwi kufanya wakati unapochagua mavazi ya kwenda nayo.

USIVAE NGUO NYEUPE
Nguo nyeupe mara nyingi inakuwa maalum kwa bwana na bibi harusi. Unapovaa unaweza kuleta gumzo kwenye sherehe yao kwa kuonekana unafanana nao.
Unatakiwa kuvaa nguo ya rangi ya maziwa, blue au rangi yoyote mchanganyiko.

USIVAE VIATU VIREFU
Usithubutu kuvaa viatu virefu usivyoweza kuvimudu, maana kwenye harusi kuna shuhuli nyingi ambazo zitakuhitaji kukaa na kunyanyuka kila mara. Viatu virefu havitakupa nafasi ya kufanya hivyo, badala yake unaweza kuichukia sherehe wakati wewe mwenyewe umefanya makosa katika uvaaji wake.

USIVAE MAVAZI YASIYOFAA
Hakikisha nguo unazovaa haziachi wazi sehemu kubwa ya mwili, hata kama nguo imekupendeza vipi lakini inapokwa wazi sana inaweza kusababisha gumzo na watu kuacha kufuatilia matukio ya harusi na kukuangalia wewe.
Jaribu kujiangalia kwenye kioo kabla ya kutoka, jaribu kukaa na kusimama ili kuona vazi lako linafaa katika watu wengi.

URE MBO



# PAMBA ZA MASIKIO
## Ni hatari kusafishia, wengi kuwa viziwi

KILA mtu anakabiliwa na tatizo la kujaa kwa utando mzito ndani ya masikio unaofanana na nta.

Kitaalam mwili wa binadamu uzalisha nta kwenye masikio kama kinga dhidi ya vijidudu, bacteria au uchafu unaoweza kuingia ndani. Hata hivyo wakati mwingine huzalisha nta kwa wingi na kusababisha usumbufu.

Nta unapozidi ndani ya sikio, mtu anaweza kupata matatizo ya kutosikia au usikifu hafifu. Inapofikia katika hali hiyo ni muhimu kusafisha masikio ili kurudisha hali yako ya kawaida.

Hata hivyo, unatakiwa kuwa na tahadhari kubwa wakati unaposafisha masikio, kwa ajili ya kuepuka madhara kama ukiondoa nta wote.

Je njia sahihi ya kusafisha masikio ni zipi? Ebu fuatilia njia hizi ili upate ufahamu wa namna bora ya kusafisha.

**PAMBA ZA MASIKIO**

Pamba iliyowekwa kwenye vijiti haifai kusafishia masikio. Bei yake ni rahisi na vinapatikana katika maduka mbalimbali yaliyo karibu.

Masikio yana kawaida ya kujisafisha yenyewe kwa kutoa nje uchafu, na upotumia vijiti kuna uwezekano wa kusukuma ndani uchafu.

Na kama ungekuwa na jicho la ndani uone unachokifanya unge acha mara moja.

Unapozidi kufanya hivi, unazidi kujaza uchafu ndani ya sikio na unavyozidi kujaa hujenga ukuta na hatimaye kuziba njia ya masIkio yako na kusababisha tatizo la kutosikia.

Unaweza tumia pamba kwa kusafishia eno la nje ya sikio lako na sio kuingiza ndani.

Pia unaonywa kutumia peni, vijiti na funguo za magari kusafishia masikio kwani ni hatari zaidi.

**NJIA SAHIHI**

Kuna njia sahihi ya kusafisha masikio bila kuleta madhara, nayo ni kutumia mafuta ya Peroksidi Hidrojeni.

Kabla ya kutumia kwanza unatakiwa kuchanganya na maji, lakini usitumie mara kwa mara kwani uweza kupausha ngozi na kuongeza nafasi ya kupata maambukizi.

Unatakiwa kupaka mara moja kwa mwezi na kama ikibidi paka mara moja mwa wiki.

Mafuta ya madini kama petrol ni mazuri kusafishia masikio, ukitumia haya mafuta itasaidia kusafisha masikio bila kuyadhuru

# MAPISHI
**Na Mary Geofrey**

## MKATE WA MAYAI

TUMEZOEA kula mikate ya aina mbalimbali inayouzwa madukani, lakini unaweza kubadilisha mlo kwa kuoka mkate wa mayai nyumbani na ukafurahia.

Mahitaji

Mayai manne, sukari vijiko viwili na nusu, unga wa ngano vijiko sita vya chakula, hiliki nusu kijiko cha chai (iliyosagwa)na backing powder nusu kijiko cha chai.

**Utayarishaji na upishi**

Chukua bakuli safi, weka sukari na hiliki, kisha vunja mayai yote juu yake.

Changanya mayai, hiliki na sukari, kwa kutumia mashine (cake mixer), mpaka sukari ivurugike na mayai yapande juu kama povu.

Paka mafuta chombo chako cha kuokea mkate na washa jiko (300-350f oven) lianze kupata moto.

Weka baking powder katika unga wako, kisha chukua mwiko na uanze kutia unga kidogo kidogo katika mchanganyiko wako wa mayai na sukari.

Hakikisha unaukoroga vizuri kila utiapo unga ili kuepusha kuwa na madonge.

Mimina mchanganyiko wako katika chombo cha kuchomea mkate.

Oka mkate wako ndani ya jiko (oven) kwa muda wa kama dakika 20 kisha utoe.

Wacha mkate upoe kisha utoe na uweke kwenye sahani safi tayari kwa kuliwa.

**Namna ya kupika mkate wa yai**

Unaweza kutupia zabibu kavu juu ya mchanganyiko wako kabla ya kuoka ili kuongeza ladha.

Hakikisha mkate wako kama umeiva vizuri kwa ingiza kijiti katikati ya mkate kisha kitoe.

Kama ukigusa kijiti na unaona ni kikavu, basi ujue mkate wako umeiva. Kama kuna ubichi basi mkate wako bado haujaiva.

Kama mkate haujaiva baada ya kukagua rudisha mkate kwa dakika tano nyingine kisha ukague tena.

Sukari ikiwa nyingi mkate wako utanata na hautaiva vizuri.



# MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**

## PAZIA KUPENDEZESHA NYUMBA



PAZIA ni miongoni mwa mapambo yanayotumika kupendezesha ndani ya nyumba.

Kama ilivyozoeleka, pazia limekuwa likitumika kupambwa mlangoni na dirishani. Katika sehemu zenye joto kali ambazo mara nyingi madirisha yake huwa yenye wavu, pazia imekuwa ikitumika sana.

Lakini hata katika sehemu ambazo madirisha yake ni yale yasiyo na wavu, bado wanatumia pazia kama pambo la kupendezesha nyumba na miaka ya hivi karibuni limekuwa likitumika zaidi kuliko miaka ya nyuma.

Si tu nyumbani, bali katika sehemu za ofisi, hotelini na sehemu zingine, pazia limekuwa likitumika kama kuziba lakini pia pambo.

Siku hizi tofauti na miaka ya nyuma, baadhi ya familia hupendelea wakati mwingine ndani ya nyumba kunapokuwa na pazia nzuri lenye mvuto, hulazimika kugharimia kuweka kiyoyozi ili pazia lisivurugike katika mpangilio wake na kuharibu mvuto wa ndani ya nyumba.

Yako mapazia yaliyotengenezwa kwa kutumia kitambaa kizito sana, ya kati na nyepesi zaidi.

Lakini pia yako mapazia ambayo yana matobo lakini yote kwa ujumla wake, yamekuwa yakitumika upamba katima nyumba, ofisi au hoteli kulingana na mahitaji au mandhari iliyoko katika sehemu husika.

Katika kutumia pambo hilo la pazia kwenye nyumba, hakikisha unachagua ambalo rangi zake inaendana na zile zilizopo katika nyumba yako.

Si lazima lifanane na rangi zote za ndani ya nyumba, lakini hata kama ni mojawapo ya yale yaliyoko ndani yatapendeza tu. Zingatia pia rangi ambazo hazing`ai sana ambazo hazileti utulivu ndani ya nyumba.



# MPANGILIO

## DONDOO MUHIMU NAMNA YA KUSAFISHA MARUMARU NDANI YA NYUMBA.

1: Fagia kila siku ili kuondoa uchafu wa juu kama vile mabaki ya vyakula au udongo.


2: Safisha kwa dekio au mopu juu ya sakafu baada ya kufagiliwa.

3: Tambaa la deki au mopu liwe safi na maji yatakayotumika yawe na sabuni kiasi.

4: Kausha sakafu baada ya kudeki kwa kutumia kitambaa kikavu au mopu iliyokaushwa.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
AMEFILISI WANAUME WENGI NA ANAENDELEA KUWAFILISI ZAIDI. KAVUNJA NDOA NYINGI SANA!
NTAJUAJE? KANIOMBEE NAMBA
KATIKA FIDIA NITAKAYOLIPWA USHATUMBUKIZA CHAKO?
ONGEA KISWAHILI FASAHA KWA SAUTI KUBWA 'CHANGU NDIO NINI?
KIINUA MGONGO NA BAR, NI KAMA UPEPO NA KIBATARI!
BABA MWENYE NYUMBA SHIKAMOO
WAPI KODI YANGU!
MKAE MKIJUA KINA'KAKA NA DADA ZAO 'WAMECHEZEA VICHAPO!
NDIO NINI?
DEREVA USHABIKI ACHANA NAO!
KWANI HANA NAFSI?
JAMANIEEE ACHENI ITUUE NI YETU SISI...
TIMU SIO DINI USEME UTABADILI LAKINI INATUTIA UNYONGE...
UNYONGE AU NYONDE NYONDE?
TUNA-DUMISHA MILA
MASHAMBA ULIYOYAUZA PESA UKAZINYWEA UNADUMISHA NINI?
HUNIKOMOI...
NAIKOMOA HIYO ILIYOKAA MFUKONI INAYOKUZUZUA KWENDA BAR.
USIPOTENGENEZA 'FITINESS' UTAJIKUTA KINA SUKARI, PRESHA NA WENZAO KAMA MIA UNAO!
MTAALAMU UNASEMA ALIYEPO HAPOI, NA AJAYE MOTO NI ZAIDI YA HUU?! RAMLI IMEONA HIVYO AU UNAJIROPOKEA?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
RAHA YA KICHEKO UWE NA MENO...

## HABARI KIMATAIFA

# Papa Francis awataka waislam, wakristo kushikamana pamoja

**BAGHDAD, Iraq**

KIONGOZI mkuu wa kanisa katoliki duniani, Papa Francis amekutana na mkuu wa madhehebu ya Shia Ayatollah al-Sistani, wamewahimiza wananchi wa Iraq kuishi kwa amani na kushikamana na wakristo ambao ni wachache nchini humo.

Papa Francis, anayefanya ziara nchini humo akiwa na kiongozi mwenzake huyo wa washia walitoa ujumbe huo baada ya kukutana na kufanya mazungumzo.

Katika ujumbe walioutowa jana, viongozi hao walitoa wito kwa waislamu kuikumbatia jamii ya wachache ya Wakristo iliyoishi katika mazingira magumu kwa kipindi kirefu. Viongozi hao wawili wakuu wa dini mbili tofauti walitowa wito huo baada ya mkutano wao wa kihistoria uliofanyika katika mji mtakatifu wa Najaf. Ayatollah Ali al-Sistani alisema mamlaka za kidini zina jukumu katika kuwalinda wakristo wa nchi hiyo wanaostahili kuishi kwa amani na kufurahia haki sawa na raia wengine.

Kiongozi huyo mwenye umri wa miaka 90, ni mmoja wa maulamaa wa juu kabisa katika madhehebu ya Shia na ni mara chache sana hujiingiza katika masuala ya kisiasa lakini uingiliaji wake wenye sauti umesaidia kuijenga upya nchi hiyo.

Pia ana mamlaka na heshima katika jamii ya Shia ambayo ndiyo walio wengi nchini Iraq, na maoni yake yanazingatiwa na kufuatwa na washia wote ulimwenguni.

Kanisa Katoliki mjini Vatican limesema Papa Francis alimshukuru al-Sistani kwa kupaza sauti yake kuwatetea wanyonge na wenye kukabiliwa na mateso katika nyakati zilizoshuhudia ghasia katika historia ya Iraq.

Mkutano wa kihistoria kati ya viongozi hao wa dini ulifanyika kwenye makazi ya al-Sistani na ulipangwa kwa miezi kadhaa.

**DW**



Kiongozi wa kanisa Katoliki duniani, Papa Francis, akizungumza na mkuu wa madhehebu ya Shia nchini Iraq, Ayatollah al-Sistani, wakati alipomtembelea nyumbani kwake mjini Najaf jana. **(PICHA:DW)**

# Ujerumani yatahadharisha Afghanistan

**BERLIN, Ujerumani**

UJERUMANI imeomba jumuiya ya kimataifa kuondoa vikosi vya majeshi ya kigeni nchini Afghanistan kwa njia salama na kwa wakati mwafaka ili kuepusha kuliacha taifa hilo chini ya mikono ya wanamgambo wa Taliban.

Kauli hiyo imetolewa na Waziri wa Mambo ya Kigeni wa Ujerumani, Heiko Maas, wakati akilihutubia Bunge la nchi hiyo siku ya Alhamisi kabla ya wabunge kuamua iwapo Ujerumani irefushe muda wa ujumbe wake nchini Afghanistan.

Maas alisema uwepo wa vikosi vya kijeshi vya kimataifa, inasalia kuwa nafasi muhimu ya kulishinikiza kundi la Taliban kushiriki kwenye juhudi za kutafuta amani kwa njia ya mazungumzoa.

Mwanadiplomasia huyo alisisitiza mazungumzo yanayoendelea kati ya serikali ya Afghanistan na kundi la Taliban inabaki kuwa nafasi adimu ya kuwezesha upatikanaji wa amani nchini humo.

Wito huo umetolewa wakati Marekani inapitia upya makubaliano yake na kundi la Taliban yaliyofikiwa mwaka jana yanayotaka vikosi vya kigeni kuondoka nchini humo Mei, mwaka huu

# Waandamanaji wauawa Senegal

**DAKAR, Senegal**

SERIKALI ya Senegal imeapa kutumia njia zote zinazohitajika kurejesha hali ya utulivu baada ya watu wanne kuuawa kwenye makabiliano makali kati ya polisi na waandamanaji.

Waandamanaji hao ambao ni wafuasi wa kiongozi wa upinzani nchini humo, Ousmane Sonko, wanapinga hatua ya serikali kumkamata na kumweka kizuizini. Akizungumza katika televisheni, Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi hiyo, Antoine Diome, alisema serikali imefadhaishwa na vifo vya watu hao na kumtuhumu Sonko kutoa wito wa kufanyika vurugu.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, alitoa wito kwa pande zote mbili kujiepusha na vurugu na kuwahimiza waandamanaji kuwa watulivu huku akiwataka maofisa wa usalama kutumia njia zinazokubalika.

Hasira ya wafuasi wa kiongozi huyo iliongezeka juzi baada ya mahakama kuamua kuongeza muda wa Sonko kuwa chini ya polisi kutokana na tuhuma za ubakaji yanayomkabili.

Mwanasiasa huyo ambaye ni maarufu hasa kwa vijana amekanusha tuhuma hizo za ubakaji.

**DW**

# Wanajeshi kuendelea kulinda Bunge

**WASHINGTON, Marekani**

WIZARA ya Ulinzi ya Marekani imesema inatafakari kurefusha muda wa wanajeshi kuendelea kuwapo katika mji mkuu wa mkuu wa Washington, kwa ajili ya kuimarisha ulinzi.

Wanajeshi hao walipelekwa katika mji huo ili kuongeza ulinzi kwenye majengo ya Bunge kufuatia uvamizi uliofanywa na wafuasi wa Rais wa zamani, Donald Trump. Msemaji wa Idara ya Ulinzi wa taifa, John Kirby, alisema wamepokea ombi rasmi kutoka polisi wakitaka wanajeshi wabakie kutoa msaada wa ulinzi kwenye majengo ya Bunge kwa miezi mingine kadhaa.

Hata hivyo, ofisa huyo hakuzungumzia sababu au kitisho kilichopo, lakini kaimu mkuu wa jeshi la polisi la Washington, aliarifu mwezi uliopita kuhusu kuwapo kwa vitisho kutoka makundi ya siasa kali yanayopanga kuzuia Rais Joe Biden, kutoa hotuba ya kila mwaka ya hali ya taifa.

Eneo la majengo ya Bunge limekuwa chini ya ulinzi mkali tangu Januari 6, mwaka huu wakati maelfu ya wafuasi wa Trump walipovamia kujaribu kuzuia wabunge kuidhinisha ushindi wa Biden katika uchaguzi wa mwaka uliopita.

SAFU

## MAKALA

# Twajaribu kujenga taifa la namna gani?



Na Magabilo Masambu

**Binafsi bado naamini hatujaenda mbali. Bado tunayo nafasi kama taifa kukaa pamoja, kujadili masuala yetu kwa pamoja. Hii ni kwa sababu nchi hii ni yetu sote, kila mmoja ana haki ya kuishi sawasawa na mwingine, bila kujali upungufu wowote wa kibinadamu alionao.**

TAIFA lolote lazima liwe na misingi imara ya kujenga watu wake kwa ajili ya vizazi vijavyo. Kuyumba kwa misingi hiyo kunaweza kusababisha nyufa katika maeneo mbalimbali kama ilivyo nyumba isiyo na msingi imara.

Kwa miongo kadhaa, Tanzania imekuwa na sifa za pekee katika maeneo mengi lakini hasa katika eneo la amani, umoja na upendo. Tofauti yetu na wengine ilikuwa kuheshimiana, kuthaminiana, kupendana lakini zaidi katika kuwa mstari wa mbele kuyaona matatizo ya wenzetu ni yetu.

Siku za hivi karibuni tumekuwa na utamaduni mpya ambao nadhani, kama hapatakuwapo watu wa kuusemea utamaduni huu, basi tunaweza kujikuta tunapotea sana na wale waliokuwa wakituheshimu wakatudharau.

Limekuwa jambo la kawaida vijana kuwatukana wazee, wazee kuwatukana vijana, viongozi wa dini na serikali kuvutana! Nafikiri tukikaa kimya hatutakuwa tumejitendea haki. Inawezekana pakawapo upungufu kadhaa pande zote, hiyo ni kawaida kwani hatujakamilika. Muhimu zaidi ni kutafuta ufumbuzi wenye kutuleta pamoja.

Nchi hii itaendelea kuwapo wote tutapita lakini lazima tujitafakari kama nchi tutaacha taifa la namna gani? Je, tunataka tuache nchi ya watu wasioheshimiana, wasiopendana, wasio wamoja, waongo au wakweli, waoga, wanafiki au tunakusudia kujenga nchi ya wastaarabu?

Binafsi bado naamini hatujaenda mbali. Bado tunayo nafasi kama taifa kukaa pamoja, kujadili masuala yetu kwa pamoja. Hii ni kwa sababu nchi hii ni yetu sote, kila mmoja ana haki ya kuishi sawasawa na mwingine, bila kujali upungufu wowote wa kibinadamu alionao.

Je, tunajenga taifa lisiloheshimu viongozi wa dini? Au tunajenga taifa lisiloheshimu viongozi wa serikali? Je, tunajenga taifa lisilo heshimu wazee? Tunajenga taifa la wazee wanaowachokoza vijana? Tatizo ni nini hasa? Je, ni sahihi kufumba macho na kujifanya hatuyaoni haya au ni bora tuyazungumze na kuyapatia ufumbuzi kisha tuendelee kuwa wamoja?

Tunaweza kusema sisi ni wamoja, ni kweli. Lakini kwa nini tumekuwa na mivutano tena hadharani basi? Haya tunayoyazungumza hadharani hatuwezi kuyazungumza sirini na tukayamaliza? Maana bahati mbaya nyingine ni kwamba mambo ya sirini siku hizi tunayazungumza hadharani na ya hadharani tunataka yawe sirini.

Utamaduni niliolelewa pengine na wengi wetu. Ilipotokea nyumbani amekuja mgeni, sisi watoto tulifanya chochote, kusimama hata kwenye sahani ya ugali! Na wazazi walionekana wapole kama hawaoni hivi, sasa ngoja mgeni aondoke ndiyo utajua kwa nini punda hajasoma lakini hakosi kazi ya kufanya!

Hata ilipotokea wazazi wakatofautiana na pengine kupigana, mara tu mgeni alipobisha hodi, wote walijitokeza sebuleni kila mmoja akitabasamu, ili kutokuonyesha tofauti zao mbele ya mgeni na kwa kweli mgeni aliondoka bila kufahamu kama muda mfupi uliopita walikuwa wakipigana.

Baada ya mgeni kuondoka ilikuwa ama wanapatana kabisa au wanarudi ulingoni mpaka mshindi apatikane. Maana yangu ni kwamba kama kuna matatizo yanayohitaji kuzungumzwa, basi itafutwe nafasi ya kuonana na kuzungumza kisha unatolewa msimamo wa pamoja kwa nia njema kabisa.

"Ni kweli kwamba demokrasia haiwezi kudumu ikiwa wachache hawatakubali matakwa ya wengi, lakini matakwa ya wengi hujulikana katika majadiliano au mazungumzo ya waziwazi. Kadhalika, matakwa ya wachache hujulikana katika majadiliano na mazungumzo. Bila wale wachache kusema waziwazi matakwa yao majadiliano hayana maana"(JK.Nyerere, 1962, Tujisahihishe)

Tukijenga utamaduni wa majadiliano katika vikao, hakuna jambo litaharibika. Mara nyingi kwenye majadiliano wazo zuri huwa linatokana na mtu mmoja tu na baadaye kuungwa mkono na wengine lakini baada ya kuliweka wazi nia na sababu ya kufanya hivyo.

Tujenge taifa linaloamini katika nguvu ya hoja na si hoja ya nguvu. Taifa linaloamini kwamba utatuzi wa mambo yetu ni kupitia katika majadiliano na mazungumzo kuliko njia nyinginezo. Taifa litakaloamini katika uamuzi wa vikao unaotokana na ujengaji wa hoja imara. Taifa la watu wanaojiamini kusema lolote bila kuvunja sheria.

Mwisho niweke wazi kwamba simlaumu yeyote. Ninachojaribu kusema ni kwamba turudi kwenye misingi yetu na utamaduni wetu wa kuheshimiana, kupendana na kushirikiana. Yaliyopita si ndwele tunaweza kufungua ukurasa mpya.

Vijana tukaanza kuwaheshimu wazee, wazee wakaacha kuwachokoza vijana, viongozi wa serikali na dini pia mkakaa pamoja, kuona tatizo liko wapi kama ndugu wamoja mkakubaliana nini cha kufanya ili nchi isiendelee kufukuta.

**Mungu ibariki Afrika, Mungu ibariki Tanzania. 0689157789 magabilomjalifu@gmail.com ARUSHA-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Enzi za Jitu lishibalo Power Mabula, TX Chaka wa mieleka



Na Adam Fungamwango

**Mieleka nayo ikaanza kushika chati nchini. Nayo ikaanza kutoa wanamieleka wazuri na waliotokea kuwa maarufu nchini Tanzania wanaokumbukwa mpaka sasa. Kwanza wakitaka kupigana, matangazo yanaanza kutoka kwenye magazeti. Kunakuwa na picha zao, halafu kila mmoja anampa 'mkwara' mwenzake.**

UNAFUNGUA gazeti la Mfanyakazi, unakutana na picha ya mtu mmoja mrefu, aliyejengeka vyema na kujaa misuli mikononi na kifuani. Mtu huyo ana nywele nyingi zenye rasta mbili ndefu. kiunoni hadi kwenye mapaja amevaa kitu mfano wa ngozi, akijifunga mithili ya msuli mfupi mgumu na kuacha eneo kubwa la mwili wake wazi.

Chini alikuwa amevaa viatu virefu kuanzia chini hadi karibu kabisa na magoti. Halafu unakutana na maandishi ya 'Kutana na Jitu Lishibalo, Power Mabula.'

Lilikuwa ni tangazo la mbabe huyo likionyesha ni wapi siku hiyo atafanya maonyesho yake. Huyu ndiye Power Mabula ambaye hakuna mtoto, mtu mzima au kijana wa kuanzia miaka ya mwanzoni mwa 1980 hadi mwanzoni mwa 1990 ambaye hamfahamu.

Alikuwa maarufu sana kwa michezo ya kutumia nguvu. Baadhi walimwona laivu akifanya maonyesho hayo, akizunguka Tanzania nzima.

Alikuwa na uwezo wa kuizua gari aina ya Land Rover kuondoka, akitumia kamba kubwa ya katani au mnyororo kuizuia. Alikuwa pia ana uwezo wa kuzuia magari mawili aina ya Peugeot 504 au 505 kuondoka kwa wakati mmoja, moja Lilifungwa upande huu na lingine upande mwingine, yeye akiwa katikati.

Power Mabula pia alikuwa na uwezo wa kuizuia pikipiki kuondoka kwa kutumia nywele zake. Akifunga kamba kwenye pikipiki kwenye rasta zake, huku mwendeshaji akijitahidi kutia gea na kuondoka, lakini wapi.

Jitu hilo, pamoja na michezo mingi, ikiwamo kubeba mifuko kadhaa ya simenti kwa kutumia meno, alikuwa na uwezo pia wa kupitisha gari kifuani kwake bila kupata madhara yoyote. Usisahau pia na kuvunjiwa jiwe kubwa kama yale yanayopatikana Kunduchi kifuani kwa kutumia nyundo.

Ilikuwa kitu cha hatari kukiona lakini pia ni kama watu walikuwa hawaamini macho yao, lakini ni kweli mwamba huyo alikuwa anafanya kwa malipo madogo tu wakati huo kwani hata wanafunzi walikuwa na uwezo wa kwenda kulipa na kuangalia michezo hiyo. Wakati mwingine alifika hadi shuleni na kufanya michezo yake hiyo.

Huyo ndiye aliyekuwa mchezaji wa kutumia nguvu maarufu zaidi nchini Tanzania wakati huo.

Baadaye walikuja wengine, lakini hawakumfikia mwamba huyu kwa kile alichokuwa akifanya kwenye maonyesho yake na hata umaarufu.

Baadaye kukaja michezo ya kupigana, maarufu kama mieleka. Power Mabula yeye hakujishughulisha kabisa na michezo hiyo. Yeye aliendelea na michezo yake ya nguvu tu.

Mieleka nayo ikaanza kushika chati nchini. Nayo ikaanza kutoa wanamieleka wazuri na waliotokea kuwa maarufu nchini Tanzania wanaokumbukwa mpaka sasa. Kwanza wakitaka kupigana, matangazo yanaanza kutoka kwenye magazeti. Kunakuwa na picha zao, halafu kila mmoja anampa 'mkwara' mwenzake.

Yale maneno wanayotishana ndiyo yanayovuta mashabiki wengi kujazana kwenye kumbi mbalimbali kushuhudia mapambano yao.

"Njoo na jeneza kabisa, hautorudi nyumbani ukiwa hai". Mwingine naye anajibu: "Leo nitakutwanga hadi ndugu zako wakuulize, umegongwa na treni au umepata ajali ya ndege?"

Haya yalikuwa baadhi ya maneno ambayo mashabiki na wasomaji walikuwa yakiyapenda sana kuyasoma kwenye gazeti kabla ya mapambano. Kuna mtu aliniambia siku hizi michezo hiyo haipo kwa sababu eti kila mtu anataka kujifanya 'sharobaro.

Akasema hata wale wachache wanaokwenda 'gym' wanafanya hivyo ili watishe na kupiga watu mitaani, wakae milangoni kwenye kumbi za starehe au kwenye vituo mbalimbali vya mabasi kwa ajili ya kukatisha tiketi.

Baadhi ya wanamieleka maarufu waliopata kutokea nchini ni Power Vuru Mroma, Power Bukuku 'Sumu ya Mamba', Power Savimbi, Power TX Chaka, Power Banardo 'Tai Kichaa', Power Ngeta 'Super Kibonge', Power Iranda, Power Mwanakulya.

Wengine ni Power Sangandele, Power Nyati, Power Mwanza, Power Nassor, na Power Masai ambaye ni mmoja wa waanzilishi wa michezo hii ya mieleka nchini.

Mmoja wa wanyanyua vitu vizito ambaye ameshastaafu na hakutaka jina lake lichapishwe, alisema hakuna ushirikina wowote kwenye mchezo huo wa kutumia nguvu isipokuwa ni sayansi ya akili na nguvu ndiyo inayosababisha waonekane wao ni watu tofauti.

Anasema ndiyo maana hakuna aliyesikia Power anapitisha lori kifuani kwake, mara zote ni magari ya kawaida kama vile Land Rover na magari mengine madogo ambayo yanaendana na uzito wa mhusika.

Kuhusu chakula alisema kulikuwa na uvumi kuwa wanakula chakula kingi zaidi kama vile mbuzi mzima peke yao na kila tano za ugali, kitu ambacho si kweli.

"Huo ni uroho. Power anakula chakula cha kawaida ambacho wengine wanakula, ila anashauriwa ale nyama kwa wingi, mboga za majani, maharagwe, japo atakula kwa kipimo cha juu zaidi kwa sababu anafanya kazi za nguvu na mazoezi magumu, lakini si kwa kiwango kinachozungumziwa mitaani. Maharagwe na mboga za jamani zinajenga na kulinda mwili na hiyo ndiyo inashauriwa zaidi," alisema Power huyo ambaye pia ni mwanajeshi mstaafu.

# HADITHI

MILIO mitatu ya risasi ilisikika maeneo ya Keko Bora jijini Dar es Salaam. Sauti hizo za risassi zilifanya watu kutimua mbio na kutafuta chaka la kujificha. Kila mmoja alidhani ni majambazi waliovamia kwa ajili ya kupora pesa dukani au kwenye vibanda vya mawakala wa kampuni za simu. Haikuwa hivyo. Aliyedhaniwa kuwa ni jambazi alichofanya ni kumpora mwanamke mtoto mwenye umri wa mwaka mmoja tu na kuondoka naye akiwa kwenye gari aina ya IST. Huyu jamaa aliyefanya hivyo ni nani? Ni kwa nini aliyemteka mtoto? Mtoto ni wa nani? Mwanamke aliyeporwa mtoto anamfahamu mporaji? Fuatilia kisa hiki kitamu, cha kusisimua na kuhuzunisha.

# Nina Jambo Langu-12

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

UGOMVI huu ulizuka baada ya Neema, Ester na Jerry kwenda Ubungo kumchukua mtoto Diana.

Neema aliwahakikishia usalama kuwa hatokwenda polisi kushtaki na hii ilichagizwa pia na mkasa mzima ulivyokuwa. Ni mkasa ambao hauhitaji kwenda polisi. Waliamua kuumaliza wenyewe Neema na Ester kwa msaada wa Jerry.

"Sasa nasema hivi. Mimi napiga ripoti polisi na kuwaambia kuwa mtoto amepatikana. Lakini sijui amepatikana vipi, yuko mikononi mwa mama yake na hataki kusema ameletwa vipi na ni nani aliyemkabidhi, halafu waje kukuchukua ndiyo utawaambia vizuri."

"Piga. Na mimi ndiyo nawataka hao polisi waje hapa. Na nikiondoka hapa, ndiyo hunioni tena."

"Unafikiri mimi naogopa hilo. Kama hujaniambia nani amekupa huyo mtoto, ina maana hiyo ni tiketi mimi kukuacha." Ben aliongea huku akimsogelea mkewe.

"Ndicho nilichokuwa natakа hicho."

"Nini?"

"Talaka" Kilichofuatia hakikuwa talaka. Ila ni kibao kikali shavuni kwa Neema kilichomfanya aone nyota nyota.

"Utaniambia na leo utanionyesha huyo hawara yako aliyokupa huyo mtoto."

Wakati maneno hayo yanamtoka Ben, alikuwa tayari ameshamchakaza mkewe kwa makofi manne.

Wakati huo Diana alikuwa ameshalazwa kitandani. Amelala usingizi.


Neema alilia, lakini hakujibu kitu chochote.

"Kumbe wewe mwanamke ni mbaya hivyo. Sikujua kama nimeoa mwanamke kahaba. Sasa nasema hivi. Kesho fungasha uende kwenu. Huwezi kuniletea mambo ya ajabu nyumbani kwangu."

Neema alikuwa amejikunja kama kakakuoa kutokana na kipigo, lakini aliposikia maneno hayo, aliinua kichwa chake na macho yake yaliyogeuka mekundu kwa kulia, yalimtazama mumewe Ben kwa hasira. Yalikuwa kama yanamwambia kuna kitu hukifahamu.

"Kesho nafungasha nakwenda kwetu, lakini utanikumbuka."

"Nikukumbuke wewe kahaba. Unagonganisha mtoto mmoja kwa baba wawili. Hadi wanamteka kwenda kupima DNA, halafu wanakupigia simu uende kumchukua. Siwezi kukukumbuka. Nimeamua tuachane, kesho nakupa talaka yako.



**"Kumbe wewe mwanamke ni mbaya hivyo. Sikujua kama nimeoa mwanamke kahaba. Sasa nasema hivi. Kesho fungasha uende kwenu. Huwezi kuniletea mambo ya ajabu nyumbani kwangu."**

******************************

"Wazee na ndugu wote. Kwanza samahani sana kwa kukukatishieni shughuli zenu kwa siku ya leo. Nimewaita hapa kukwambieni kuwa ndugu yenu ameniacha." Neema alinyamaza kidogo na kuwafanya watu waliokuwepo pale kuonyesha mshangao, ingawa wengi wao walishajua sababu za kuitwa kwenye kikao hicho.

"Ndugu yenu amenipa talaka juzi na tumekwenda Bomani kuthibitisha kuwa ndoa hii haipo tena. Leo na ninyi ndugu za mwanamume na ndugu zangu ambao kwenye kikao hiki wako wawili tu. Hapa nimewaita kwa mambo mawili. Kwanza kabisa, kama linaweza kusuluhishwa hili lisuluhishwe. Lakini kama haliwezekani, basi mimi niondoke, lakini wakati kila mtu akijua nani ana makosa."

Kilikuwa ni kikao cha wanafamilia. Ndugu wa Benson ambao ndio walikuwa wengi kwenye kikao hicho na ndugu wawili tu wa Neema walikutana.

Tatizo lilikuwa ni lile lile. Ben na ndugu zake walitatizwa mno na mkasa mzima wa mtoto kutekwa, halafu kukaa huko mwezi mzima bila taarifa, baadaye anakutwa mikononi mwa mama mtu kirahisi tu bila tatizo lolote.

Si Ben tu, hata ndugu zake waliamini kuna kitu ambacho si kawaida. Na moja kwa moja dhana ilikuwa huenda aliyemteka mtoto alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Neema kabla au baada ya ndoa. Inawezekana ikawa mimba ilipatikana wakati Neema ana wanaume wawili, mume na mchepuko, hivyo jamaa akawa anahitaji mtoto wake na mwisho akaamua kumteka.

Ndugu wa Ben na mwenyewe walishakaa vikao na kufikiri hilo.

Kilichowasukuma wahisi hilo zaidi ni jinsi mtoto huyo alivyokaa kusikojulikana mwezi mzima bila mtekaji kueleza sababu, au kutaka pesa.

Imani ilikuja na kuamini walichoamini pale walipoona mtoto amerejeshwa kwa mama yake na hakukuwa simu iliyopigwa au kitu chochote kile, badala yake tu wakamuona Neema ana mtoto na yeye mwenyewe hataki kusema jinsi alivyompata na wapi amempata na nani aliyempa.

Uhai wa ndoa iliyodumu kwa miaka mitatu ya Ben na Neema sasa ulikuwa shakani.

Ilikuwa wakati wa Ben naye kutoa aliyo nayo moyoni baada ya Neema kuongea.

"Mimi sina la kuongea. Yote yaliyotokea kwa siku za karibuni mmeyashuhudia. Kusema kweli nimekwazika na nimetiwa aibu. Yamenichosha, hivyo nimeamua nilichoamua. Na mimi wala sikutaka kikao chochote." Alisema akionekama mnyonge na mchovu.

"Kaka na wewe tulikwambia? Ulikuwa na mke tayari unakwenda kuvamia wasichana wengine siyo." Ilikuwa ni sauti ya Edita. Dada wa Ben, akimlaumu kaka yake.

"Na kweli si bora tu umrudie mkeo? Tena yule mlifunga ndoa ya kanisani bado ipo tu." Alidakia dada mwingine.

Wakati huo ndugu wa kiume wa Ben walikuwa kimya. Hawakutaka kuingilia sana suala hilo. Hawakutaka pia kubadilisha kile ambacho kimefanywa na ndugu yao kwa sababu kila kitu wanakifahamu.

"Naona hapa kila mtu ananilaumu mimi. Na mimi ndiyo naonekana mkosaji ninayestahili kuadhibiwa kwa kupewa talaka kwa sababu ya kutekwa kwa huyu mtoto na jinsi alivyopatikana. Naonekana sikuwa mwanimifu kwenye ndoa. Kila mtu anadhani kuwa aliyemteka Diana ni hawara yangu na ndiyo maana amerudishwa kirahisi, eti mimi nimekwenda kumwomba kwa kulinda ndoa. Hii si kweli." Neema aliendelea kuiambia hadhara.

Maneno aliyokuwa anaongea tayari yalikuwa yameshazoeleka. Ndiyo ambayo yamesababisha apewe talaka. Yalianza kuwachosha waliohudhuria. Wao walidhani kuna kipya ambacho hawakijui. Walitaka amalize akusanye virago vyake na wao kila mmoja aende kwenye shughuli zake.

"Baba Diana majuzi alinitaka nimtaje mtu ambaye alimteka mtoto. Sasa leo hii nimleta kabisa hapa hapa aliyemteka mtoto huyu. Sasa kama mtamkamata sawa, au sijui mtaelewana naye vipi mtajua mwenyewe." Ni maneno ambayo yalimshtua kila mtu.

Kwa jinsi walivyofikiria. Hakuna hata siku moja waliyoamini hata kumsikia, achilia mbali kumuona mtu huyo aliyemteka mtoto.

"Utamleta kwenye kikao kijacho au?" Aliuliza mmoja wa wanandugu.

"Hapa hapa, ameshafika yupo nje hapo."

Kila mmoja sasa alipigwa na mshangao pamoja na mshawasha wa kutaka kujua nini kinaendelea. Mtekaji kujileta mwenyewe. Tena kwenye kikao ambacho ndugu wote wamekusanyika, lilikuwa jambo la kufikirika zaidi na si la kiuhalisia.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# CAREEN AWASHANGAA WANAUME BAHILI

CAREEN Simba ambaye ni mama mtoto wa mwanamuziki wa Bongo Fleva, Barakah The Prince, amesema mwanamume kutoa pesa kwa mpenzi wake ni jukumu lake ili kumlinda na wanyatiaji.

Mrembo huyo ambaye anapamba video za wanamuziki, amesema kuachana kwake na Barakah ni kutokana na Naj kuingilia kati penzi lao na sio kwa sababu hakumpatia pesa za matumizi.

"Mwanamume kumpa pesa mwanamke ni jukumu lake kwa kweli, lazima umhudumie ingawa na yeye anatakiwa afanye kazi sio kila kitu mpaka amwambie mwanamume wake," amesema Careen.



# SIKIA MPYA YA GIGY MONEY

WAKATI kesho ni kilele cha Siku ya Wanawake duniani, msanii wa muziki wa kizazi kipya, Gigy Money amefunguka akisema uoga wake umemfanya kuwa mtu maarufu.

Akizungumza na EATV, Gigy amesema alipoanza kuingia katika sanaa mama yake alimzuia, lakini aliamua kutoroka nyumbani kutokana na kuwa na hofu.

"Nilizuiliwa na mama yangu kuwa mwigizaji, nikaondoka nyumbani kwake na sikurudi, niliona nimekosea tayari na nahisi nilimwonyesha dharau ambayo sijawahi kumfanyia, uoga wangu ulinifanya nizidi kuwa Gigy Money na kuwa mtu maarufu " amesema Gigy Money

# Dicky Flavour kutoa nyingine kali

MSANII anayechipukia kwa kasi wa Bongo Fleva, Dicky Flavour, amesema hivi karibuni atakamilisha ngoma yake mpya.

Akizungumza na Gazeti hili, Dicky Flavour, amesema ameanza kazi ya kurekodi katika studio moja na anatarajia ndani ya miezi miwili ataitambulisha kwa mashabiki wake.

"Baada ya wimbo wangu 'Tuyamalize' kufanya vizuri kwa upande wangu sijapoa, hivi sasa nipo katika mchakato wa kufanya kazi ya pili naamini itakapokamilika itakuwa kali sana," amesema Dicky Flavour.



HABARI MICHEZO




# OSCAR
## ATAMANI KURUDI CHELSEA

**LONDON, China**

NYOTA wa zamani wa Chelsea, Oscar, ameelezea hamu yake ya kutaka kurudi Stamford Bridge baada ya kuondoka kwa kipindi cha miaka minne.

Oscar aliondoka Chelsea kwa uhamisho wa pauni milioni 60 na kwenda kujiunga na Klabu ya SIPG inayoshiriki Ligi Kuu nchini China.

Oscar ameiambia talkSPORT: "Nafikiria kumaliza soka langu Chelsea kwani nilikuwa na wakati mzuri hapo awali.

"Chelsea ilinisaidia sana kuboresha na kufanya kile nilichokuwa nikiota kucheza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na walinisaidia kucheza Kombe la Dunia na kushinda Ligi Kuu England.

"Nina marafiki wengi Chelsea, ikiwa nina nafasi ya kumaliza kazi yangu huko, ni ndoto kwangu.

"Kwa kweli, Chelsea haipendi kununua wachezaji wengi wakubwa, ambayo ni kawaida kwa sababu ni timu ya juu kutoka Ulaya, lakini nitajitahidi kadri niwezavyo kuwa fiti kumaliza soka langu pale."

# MESSI KUJADILI MKATABA MPYA




**BARCELONA, Hispania**

NYOTA wa Barcelona, Lionel Messi, amekubali kufanya mazungumzo na timu hiyo juu ya mustakabali wake wa kubakia klabuni hapo wiki ijayo.

Nyota huyo raia wa Argentina mwenye umri wa miaka 33 mara kadhaa amekuwa akitangaza hadharani kiu yake ya kuikacha miamba hiyo ya soka la Hispania.

Lakini wadadisi wa mambo wanasema kitendo hicho cha kukubali kufanya nao mazungumzo ni hatua nzuri ya kubakia klabuni hapo.

Nyota huyo anataka hadi mchakato wa kumpata rais wa klabu hiyo umalizike kwanza kwenye uchaguzi unaofanyika leo Jumapilii ndio aanze kujadili suala la mkataba mpya.

Mkataba wa Messi utamalizika mwishoni mwa msimu huu na klabu kadhaa zikiwamo PSG na Manchester City zimekuwa zikipigana vikumbo kuwania saini ya nyota huyo.

# TUCHEL AITABIRIA MAKUBWA CHELSEA

**LONDON, England**

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, anaamini kwamba, The Blues hao wanaweza kuleta ushindani mkali kwenye mbio za kuwania taji la Ligi Kuu England msimu ujao.

Msimu huu Chelsea imekuwa ikisuasua katika mbio hizo na sasa ipo nafasi ya nne katika msimamo wa ligi hiyo.

Manchester City wapo juu katika jedwali la Ligi Kuu England kwa tofauti ya pointi 14 katika harakati za kutwaa ubingwa, wakati Chelsea wapo kwenye kupambania kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Chelsea ya Tuchel iko nyuma kwa pointi 21 City ya Pep Guardiola, ikiwa imemaliza alama 33 nyuma ya mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Liverpool mwaka 2019-20.


Chelsea imekuwa ikijitahidi kushindania taji hilo tangu ilipofanya hivyo msimu wa 2016-17.

Lakini Tuchel ambaye ni kocha wa zamani wa Paris Saint-Germain, akiwa amechukua mikoba ya kukinoa kikosi hicho kutoka kwa Frank Lampard Januari, mwaka huu ana imani kuwa Chelsea inaweza kufikia kiwango kilichowekwa na City na Liverpool msimu ujao.


"Ukisoma namba hizi kwa sauti kubwa basi inaonekana sio," alisema Tuchel akinukuliwa na Sky Sport.

"Lakini hatupaswi kupunguza mawazo yetu. Tunapaswa kujaribu na sio kujiandaa kwa visingizio.

"Kiasi cha alama kinaonyesha jinsi pengo lilivyo kubwa. Lakini lazima iwe matarajio ya kuipunguza haraka iwezekanavyo.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HENDERSON LANGONI UNITED IKIIVAA CITY

Golikipa huyo atashuka kwa mara ya nne msimu huu baada ya De Gea kukabiliwa na...

**MANCHESTER, ENGLAND**

GOLIKIPA, Dean Henderson ataanza kwenye mchezo wa 'dabi' ya Manchester itakayochezwa leo, Kocha Ole Gunna Solskjaer amesema.

Manchester United itakuwa kwenye dimba la Etihad katika mechi ya Ligi Kuu England kupambana na majirani zao Manchester City ambao ndio vinara wa ligi hiyo.

Solskjaer amethibitisha golikipa namba moja, David de Gea hatokuwapo kwenye mchezo huo, kwani atakuwa na familia yake baada ya mke wake kujifungua mtoto wake wa kwanza.

De Gea alikosa pia mchezo dhidi ya Crystal Palace siku ya Jumatano usiku, baada ya kuomba ruhusa ya kusafiri kwenda nchini Hispania ili kuwa karibu na mke wake Edurne aliyekuwa akitarajia kujifunga mtoto ambaye wamempa jina la Yanay.

Raia huyo wa Hispania ataendelea kuwa na familia yake kwa muda aliopewa na Henderson anajiandaa kucheza mchezo wake wa nne wa ligi kwa msimu huu.

United wataingia kwenye mchezo huo wakiwa na harakati za kumaliza uteja wa kufungwa na City ambao hawajafungwa katika michezo 21 mfululizo.

Solskjaer alitoa taarifa juu ya kukosekana kwa De Gea wakati akizungumza na waandishi wa habari Ijumaa.

"Ni siku ya kupendeza kwa David. Unapokuwa baba labda ndio hisia nzuri zaidi unayoweza kuwa nayo.

"Nitampa muda anaohitaji kabla ya kurudi, aliuliza hukusu kurudi nyumbani na katika ulimwengu wa zamani atarejea akiwa yuko tayari tena.

"Na kwa wakati huo, Henderson atakuwa golini kubeba majukumu yake, naamini atakuwa na wakati mzuri."

## KWA UFUPI

**TAPSOBA ANUKIA UNITED**
MANCHESTER United imekuwa ikimfuatilia mlinzi wa kati wa Bayer Leverkusen na Timu ya Taifa ya Burkina Faso, Edmond Tapsoba mwenye umri wa miaka 22. **(Express)**

**BAILEY AGEUKA LULU**
KLABU ya Manchester United pia imefanya mazungumzo kuhusu fowadi wa Leverkusen na Jamaica, Leon Bailey mwenye umri wa miaka 23, ambaye pia anawaniwa na Tottenham Hotspur na AC Milan. **(Express)**

**TRAORE SOKONI**
KLABU ya Wolverhampton Wanderers itasikiliza ofa kwa klabu itakayomtaka, Adama Traore mwenye umri wa miaka 25 ifikapo mwishoni mwa msimu huu. **(Mail)**

**CHELSEA MATUMAINI**
CHELSEA ina imani itashinda kwenye mbio za kumsajili straika wa Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20, kutoka Borussia Dortmund kipindi cha majira ya joto. **(Metro)**

**MADRID YAIHOFIA CITY**
REAL Madrid inaamini Manchester City itakuwa kikwazo kikubwa kwenye mbio za kumsajili Erling Haaland mwenye miaka 20 ambaye ada yake inatajwa kuwa pauni milioni 100. (**AS, via Mail)**

**BAYERN VS HAALAND**
RAIS wa Bayern Munich, Herbert Hainer amesema miamba hao wa Ligi Kuu Ujerumani maarufu Bundesliga, watakuwa na nguvu ya fedha kupambana kwenye mbio za kuwania kumsajili, Erling Haaland. **(Mirror)**

**LIVERPOOL KUKIMBIWA**
KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amesema kwamba, kama wakishindwa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao, wachezaji wengi wataihama klabu hiyo.**(Mail)**

**LAMPTEY AKARIBIA CHELSEA**
CHELSEA bado inaendelea kuwania kumsajili mlinzi wa Brighton mwenye umri wa miaka 20, Tariq Lamptey, ambaye pia anawaniwa na Arsenal. **(Sun)**

**TAVARES AWINDWA**
BURNLEY na Newcastle United zinamfuatilia kwa karibu mlinzi wa Ureno, Nuno Tavares, huku timu ya Napoli ya Italia pia ikionyesha nia ya kumtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 anayeichezea Benfica player. **(O Jogo)**



## HABARI MICHEZO

# MGOSI AIPONDA YANGA PRINCESS, AONGOZA LIGI

**Na Saada Akida**

BAADA ya timu yake kuibuka na ushindi mnono wa mabao 3-0 dhidi ya watani zao, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi' amesema kikosi cha Yanga Princess kinacheza soka la 'kubutua butua' kama wanavyocheza kaka zao, Yanga kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ushindi huo umeifanya Simba Queens kufikisha pointi 39 na kukaa kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania huku Yanga Princess ikiteremka hadi kwenye nafasi ya pili ikiwa na pointi 38.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mgosi alisema timu yake imepata ushindi kwa sababu ni bora huku 'akiwananga' Yanga Princess kwamba uchezaji wao hauna tofauti na timu kubwa.

Kiungo huyo wa zamani wa Simba na DC Motema Pembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), alisema wachezaji wake walitulia na walicheza soka ambalo asili ya timu hiyo hucheza kwa miaka yote.

Mgosi alisema alikuwa akiwafatilia wapinzani wanapocheza na kuangalia upungufu na ubora wao hali ambayo waliifanyia kazi na kutumia upungufu huo kupata ushindi huo.

"Yanga Princess hii haina tofauti na kaka zao, kwani ukiangalia mpira wanaocheza ni ule wa kubutua butua, nililijua hilo na niliongea na wachezaji wangu kutaka kucheza soka halisi la Simba, hivyo tumefanikiwa kwa kipindi cha kwanza kufunga mabao 3-0,".

"Pia matokeo ya sare dhidi ya Ruvuma nayo ilitufanya tukae chini na kujiuliza upungufu wetu ambayo tuliyafanyia kazi, nawapongeza wachezaji wangu kucheza kwa maelekezo ambayo tumewapa kama benchi la ufundi," alisema Mgosi.

Aliongeza malengo yao yalikuwa ni kupambana kupata matokeo mazuri ili kupanda katika msimamo wa ligi hiyo na kuendelea kujiimarisha kwenye mbio za kutetea ubingwa wa ligi hiyo wanaoushikilia.

Naye Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Edna Lema, alisema wamepoteza mchezo dhidi ya timu bora na katika kipindi cha kwanza wachezaji wake hawakucheza mpira mzuri huku wakifanya makosa mengi ambayo wapinzani wao waliyatumia na kupata mabao ya kuongoza.

Edna alisema anawapongeza Simba Queens kwa kutumia vizuri upungufu wao na kipindi cha kwanza walikuwa bora zaidi kwa sababu walitengeneza nafasi nyingi za kufunga mabao.

"Niwapongeze Simba walikuwa bora kipindi cha kwanza lakini tulikuja kugawana kipindi cha pili tulicheza mpira, hivyo niliingia na mfumo wa kuzuia ambao haukuwa na faida kwetu kwa kumwacha mshambuliaji mmoja mbele,."

"Kuhusu kadi nyekundu ilituathiri kwa upande wangu ilikuwa halali kwa sababu mchezaji alizuia mpira kwa mikono ili mpira usiingie golini, bado hatujakata tamaa kuhusu mbio za ubingwa nina imani kuna mechi nyingi na tutafanya vizuri," aliongeza kiungo huyo wa zamani wa Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars).



Mshambuliaji wa Simba Queens, Mwanahamisi Omary 'Gaucho' (katikati), akimiliki mpira huku akiwa amezungukwa na wachezaji wa Yanga Princess katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi. Simba Queens ilishinda mabao 3-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Hard Rock yarejesha matumaini

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BAADA ya kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Kipanga, mabosi wa Hard Rock, wamesema timu hiyo itaendelea kupambana kuhakikisha inabakia kwenye Ligi Kuu Zanzibar katika msimu ujao.

Kocha Msaidizi wa Hard Rock yenye makazi yake kisiwani Pemba, Vuai Silima, aliliambia gazeti hili jana ligi imekuwa ngumu na yenye ushindani zaidi lakini timu yao haitakata tamaa na imejipanga kupambana hadi mechi ya mwisho ya msimu.

Silima alisema nguvu zao watazielekeza zaidi katika kuhakikisha hawapotezi mechi yoyote ya mzunguko huu wa lala salama na kwa kufanya hivyo watatimiza lengo lao la kubakia kwenye Ligi Kuu Zanzibar. Alisema kilichochagia timu hiyo kufanya vibaya katika mzunguko wa kwanza ni kutofanya vizuri usajili ambapo kipindi hicho wachezaji walikuwa wanaangalia maslahi zaidi na hivyo timu yao ilikosa nyota sahihi iliowahitaji.

"Tulifanya makosa kidogo katika dirisha kubwa, lakini katika dirisha hili dogo timejaribu kujaza nafasi ambazo tunaona zitaisaidia timu kufanya vizuri na kulinda daraja tulilopo," alisema Silima.

Hata hivyo kiongozi huyo aliwataka mashabiki na wachezaji wa timu hiyo kutovunjika moyo na matokeo waliyoyapata katika mzunguko wa kwanza na anawakumbusha kuongeza juhudi na ushirikiano kwa ajili ya kufikia malengo.

Katika mechi ya juzi jioni, Hard Rock ilifanikiwa kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya 'ndugu zao' Kipanga katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Gombani na kufikisha pointi 11 lakini ikiendelea kuburuza mkia.

# KVZ haikamatiki Ligi Kuu Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA Mkuu wa KVZ inayoshiriki Ligi Kuu Zanzibar amesema kikosi chake kitaendelea kusaka matokeo chanya katika kila mchezo ili lengo lao la kutwaa ubingwa wa ligi hiyo msimu huu litimie.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa KVZ, Sheha Khamis alisema ameendelea kukiimarisha kikosi chake na wamejipanga kutumia mbinu nzuri zaidi ambazo anaamini zitawasaidia ushindi katika mechi kwenye mzunguko huu wa lala salama.

Sheha alisema timu zote hivi sasa zinacheza soka lenye kasi na ili kuvuna pointi ni lazima kuwasoma vyema wapinzani kabla na baada ya mechi kuanza.

Kocha huyo alisema timu zote pia zimefanya usajili mzuri katika kipindi cha dirisha dogo na marekebisho hayo yamechangia kuongeza ushindi tofauti na ilivyokuwa kwenye mzunguko wa kwanza.

"Ligi ngumu sana, ushindani ni mkubwa, tofauti na mashabiki wanavyoitazama, tupo katika mzunguko wa pili, lakini anayeongoza ligi hata alama 30 hajafikisha, ina maana mpaka sasa hatuwezi kutabiri bingwa atakuwa nani na wala anayeshuka daraja ni nani," Sheha alisema.

KVZ iliondoka na pointi tatu baada ya kupata ushindi wa bao 1-0 katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar dhidi ya Chuoni iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mau B juzi wakati katika Uwanja wa Mau A, 'Maafande' wa Polisi na Zimamoto waligawana pointi baada ya kutoka sare ya goli 1-1 huku KMKM ikipunguzwa kasi ya kuwania ubingwa baada ya kuchapwa mabao 2-1 na Mafunzo.

Ushindani kwenye Ligi Kuu Zanzibar 'umeamka' upya baada ya Mrajisi wa Vyama vya Michezo Visiwani hapa, Abubakar Lunda kufuta kauli iliyotolewa na Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), juu ya mabadiliko ya kanuni ya Mashindano ya msimu wa mwaka 2020/21.

Lunda alisitisha uamuzi uliotolewa na ZFF wa kuongeza idadi ya timu zitakazoshiriki Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao na msimu huu kutokuwa na timu zitakazoshuka daraja.

Kauli hiyo ililalamikiwa pia na wadau ambao walisema ligi imepoteza ushindani na mvuto huku timu ambazo zilikuwa kwenye hatari ya kushuka daraja zikiendelea kubweteka na vita ilibakia kwa klabu zilizokuwa zinawania ubingwa pekee.

# Michezo

Jumapili Machi 7, 2021

Nipashe




## Henderson langoni United ikiivaa City

HABARI UK 22

## Polisi TZ, Yanga vita ya heshima

**Na Saada Akida**

MBIO na vita ya kuwania ufalme wa nchi inatarajia kuendelea tena leo kwa Polisi Tanzania kuwakaribisha vinara Yanga katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Yanga itashuka uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya kupoteza pointi tatu baada ya kukubali kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Coastal Union ya Tanga wakati Polisi Tanzania waliifunga KMC FC goli 1-0.

Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze aliiambia gazeti hili amelazimika kubadilisha mbinu za kimchezo kwa ajili ya kupata matokeo mazuri na kuendelea kujiimarisha katika msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 12.

Kaze alisema bado timu yake ina nafasi nzuri ya kupata matokeo chanya katika mechi hiyo baada ya kurekebisha makosa ambayo yalijitokeza kwenye mechi za nyuma.

Alisema aligundua mapungufu mbalimbali na kuyafanyia kazi ili kuwa bora na imara katika mechi zinazofuata na atаingia na mbinu tofauti alizozitumia kwenye mechi dhidi ya Coastal Union ambayo walipoteza.

"Bado tuna nafasi ya kufanya vizuri, tumejiandaa na tumesharekebisha makosa yetu kuelekea mechi hii, malengo yetu ni kuhakikisha tunapata pointi tatu dhidi ya Polisi Tanzania,".

"Ni mechi ngumu na itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu kila mmoja anahitaji kupata matokeo kwa ajili ya kukaribia malengo yake, pia wenzetu wako nyumbani na wanahitaji kukamilisha hesabu wakati ligi ikielekea kwenye hatua za lala salamai," alisema Kaze.

Naye Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, Hamsini Malale alisema ushindi walioupata dhidi ya KMC umewapa nguvu na kupambana kwa ajili ya 'kuwasimamisha' Yanga ambayo awali ilikuwa timu pekee ambayo haijapoteza mechi.

"Hakuna mechi rahisi kwetu, Yanga wako vizuri, tunawaheshimu, tumejipanga kuhakikisha tunafanya vizuri kwa kuzuia pointi hasa tunapocheza nyumbani bila kujali tunacheza na timu gani, tunachohitaji ni kupata pointi tatu muhimu kwa kila mechi," alisema Malale.

Yanga bado inaongoza ligi hiyo ikiwa na pointi 49 baada ya kucheza michezo 22 wakati wenyeji Polisi Tanzania walioko katika nafasi ya nane kwenye msimamo wana pointi 28.



Kiungo wa Simba, Rally Bwalya (katikati), akijipanga kuwatoka wachezaji wa Al Merrikh, katika mechi ya Kundi A ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, iliyochezwa kwenye Uwanja wa Al Hilal jijini Khartoum, Sudan jana. Timu hizo zilitoka suluhu. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA SC YAZIDI KUTAKATA AFRIKA

●●●Ni baada ya kulazimisha sare ugenini Sudan na kuendelea kuongoza katika Kundi A...

**Na Adam Fungamwango**

WAWAKILISHI wa Tanzania katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba, walilazimisha suluhu dhidi ya wenyeji Al Merreikh kwenye mechi ya Kundi A ya michuano hiyo iliyochezwa ugenini jijini Khartoum nchini Sudan jana.

Ilionekana kama Simba waliihitaji zaidi suluhu hiyo kuliko Al Merrikh kwa sababu walicheza kwa taratibu zaidi, huku wapinzani wao wakilazimisha kufanya mashambulizi, hasa kupitia kwenye winga za pembeni kutokana na wachezaji wao kuwa na kasi.

Kwa matokeo hayo, Simba bado inaongoza kundi hilo ikifikisha pointi saba, bila kujali matokeo ya mechi kati ya Al Ahly ya Misri dhidi ya AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC)iliyopigwa jana usiku.

Simba imekuwa na matokeo mazuri msimu huu baada ya kuvuna pointi nne ugenini tofauti na ilivyokuwa katika msimu wa 2019, ambapo ilipoteza michezo yote mitatu ya ugenini kwa kuchapwa mabao 5-0 kwa kila mchezo.

Mechi ilianza taratibu, lakini dakika ya 12 nusura Al Merreikh ipate bao baada ya faulo iliyopigwa na Ahmed Adam kuzua kizaazaa langoni mwa Simba, lakini mpira ukatoka nje na dakika mbili baadaye Wekundu wa Msimbazi walijibu shambulizi hilo, lakini wachezaji Chriss Mugalu, Rarry Bwalya na Luis Miquissone wakajigongagonga na kushindwa kuuweka mpira wavuni.

Mchezaji Darren Edjomariegwe aliikosesha Al Merriekh bao dakika ya 18, aliporuka juu kuunganisha mpira wa faulo na kutoka nje kidogo ya lango la Simba.

Simba ilinusurika tena kufungwa kutokana na kona iliyopigwa dakika ya 28, ikaleta kizazaa na kuwagonga mara mbili wachezaji wa Al Merreikh, lakini mpira ulikataa kuingia wavuni.

Faulo ya Clatous Chama dakika ya 42, nusura iingie nyavuni kama si umahiri wa kipa, Munjid Al Neel. Kipindi cha pili kwa nyakati tofauti, Simba iliwatoa Bwalya, Mzamiru Yassin, Chama na Mugalu na nafasi zao kuchukuliwa na Erasto Nyoni, Francis Kahata, Hassan Dilunga na Meddie Kagere, lakini uchezaji wa Simba haukubadilika.

Kuna wakati wachezaji wa Simba walikuwa wanapiga mipira mirefu ya juu, lakini Kocha Mkuu Didier Gomes alipiga kelele ya kuwatakaza, akitaka wacheze pasi fupi fupi ili mradi tu muda usogee ili kulinda angalau pointi moja.

Dakika 10 za mwisho, mashabiki wa Simba walikaa roho juu kutokana na Al Merreikh kuonekana kucharuka na kupata faulo tatu za hatari karibu kabisa na lango, lakini walishindwa kuzitumia kupata bao ambalo lingewafanya wapate ushindi wa kwanza katika hatua hiyo ya makundi.

Timu hiyo bado inaendelea kuburuza mkia, ikiwa haina pointi hata moja kutokana na mechi tatu ilizocheza, ikipoteza mbili, 3-0 dhidi ya Al Ahly ugenini na baadaye ilifungwa magoli 4-1 nyumbani dhidi ya AS Vita.

Simba itarejea nyumbani leo kwa ajili ya kuwasubiri Waarabu hao katika mechi nyingine ya hatua ya makundi itakayochezwa Machi 16, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042